# KUCHUNGUZA SHAHIDI ASIYEGAWANYIKA

Wafuasi wa Yesu,
maendeleo ya jamii,
na jamii ambazo hazijafikiwa na injili.



**Mwongozo Wa Washiriki**

# *KUCHUNGUZA SHAHIDI ASIYEGAWANYIKA*

Wafuasi wa Yesu,
maendeleo ya jamii,
na jamii ambazo hazijafikiwa na injili.

**MWONGOZO WA WASHIRIKI**

**Swahili**

# KUCHUNGUZA SHAHIDI ASIYEGAWANYIKA

## MWONGOZO WA WASHIRIKI

Toleo 3.1; Julai 2025

## Utangulizi na kanuni ya 1

**Nina tarajia kupata nini katika mafunzo haya haya ya kuchunguza mashahidi wasiogawanyika?**

Tunatamani Mungu atukuzwe: katika maisha yetu, miongoni mwa wale ambao hawajamjua bado, na kwa kweli, katika ulimwengu wote na katika uumbaji wote (Ufunuo 5:13).

Mara nyingi tunamwomba Baba yetu wa mbinguni, 'ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe'. Tunawezaje kushikilia maombi yetu? Wajumbe wa habari njema wanaonekanaje, na wanafanya nini, wale wajumbe wenye miguu mizuri wanaotangaza kwamba Mungu anatawala (Isaya 52:7)?

**Kuchunguza Ushahidi Usiogawanyika** kumejengwa juu ya kanuni kumi zilizotengenezwa katika kitabu Ushahidi Usiogawanyika: Wafuasi wa Yesu, maendeleo ya jamii, na jamii zisizofikiwa sana (Regnum 2020). Kanuni hizo ziliunganishwa na wafanyakazi wenye uzoefu wa maendeleo ya jamii wanaohudumu na OM pamoja na washiriki kutoka Kituo cha Oxford cha Mafunzo ya Misheni, Chuo cha Kikristo cha Mataifa Yote, na mashirika mengine mawili.

Kuanzia ufalme wa Mungu na jinsi tunavyouingia, kanuni hizi zinapitia mada za kumtukuza Mungu kupitia utume kamili. Majadiliano ya vita vya kiroho yanafuatiwa na kiungo cha kutunza uumbaji na hitaji la kuwa na nia thabiti katika ushuhuda wetu usiogawanyika. Haja ya weledi katika maendeleo ya jamii inaambatana na kanuni za kupanda jamii mpya za wafuasi wa Yesu, kisha kufungwa na tafakari juu ya kwa nini wale wasiofikiwana injili mara nyingi hupuuzwa.

Kozi hii imeundwa kwa wiki kumi na moja: moja kwa kila moja ya kanuni kumi, kisha kipindi cha mwisho cha kuzingatia yale tuliyojifunza, yale tunayotaka kuendelea kujifunza bado, na jinsi tunavyoweza kusonga mbele. Kiini cha vipindi vya kila wiki kinapaswa kuchukua kama dakika 75; tunapendekeza upange dakika 90 ili kutoa muda kwa kikundi kusalimiana, kuzungumza, na kusali pamoja.

Vipindi vitaongozwa na mkufunzi; kujifunza kutatokana na tafakari na majadiliano (sio kutokana na mkufunzi). Kitabu cha ushahidi usigawanyika ni nyenzo bora; tunawahimiza wanafunzi kupata nakala na kukisoma ikiwezekana. Hata hivyo, washiriki wanaweza kukamilisha utafiti huu na kunufaika nao bila kusoma kitabu hicho.

Kwa pamoja tunapomchunguza ***shahidi asiyegawanyika***, tunatumaini kwamba utapata uelewa wa kina wa maana ya kuwa watu kamili kweli. Injili haihubiriwi tu, wala matendo mema hayafanywi kwa kujificha. Kuwa mfano na maelezo ya habari njema hayawezi kutenganishwa wala kulazimishwa katika makundi ya kipaumbele. Watu tunaowakaribia ni watu kwa ukamilifu wao; wao si miili isiyounganishwa kwaajili ya kuponywa tu au roho zao kuokolewa. Kama vile Yesu alivyofanya, tunakuja kwenye jamii kama watu kamili, au tusiwaendee kabisa.

Tunataraja  kuchunguza kwa pamoja!

Exploring Undivided Witness: Facilitator Guide © 2025 by David Greenlee and team is licensed under Creative Commons Attribution-NonCommercial-NoDerivatives 4.0 International. To view a copy of this license, visit https://creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/4.0/

Cover photograph ©Quang Nguyen Minh from pixabay.com. Other photographs courtesy of OM International by Justin Lovett, Alex Coleman, Rebecca Rempel and Garrett Nasrallah.



# Kanuni ya Kwanza: Kuuelewa ufalme wa Mungu ni jambo la msingi

Malengo ya Majadiliano haya:

1. Watu katika timu yetu watatambua jinsi Yesu alivyotumia mifano na maelezo kuwasaidia watu kuelewa ufalme wa Mungu.
2. Watu katika timu yetu wataanza kuzingatia kwa namna gani ukiuelewa ufalme wa Mungu unavyoweza kukusaidia kutengeneza huduma yako wenyewe.

## *Utangulizi wa kuchunguza Shahidi Asiyegawanyika*

1. Soma "nini cha kutarajia kutokana na mafunzo haya" kwenye ukurasa uliopita.

## Ufalme wa Mungu (dakika 15-20)

2. Tuanze kwa kuangalia Kanuni ya Kwanza.

   Muhtasari wa Kanuni ya Kwanza: *'Kuelewa ufalme wa Mungu ni jambo la msingi'*

3. Kuuelewa ufalme wa Mungu ni msingi, kwa hiyo hebu tuangalie ufalme wa Mungu ni nini. Ufalme unaweza kufafanuliwa kama mahali ambapo mfalme anatawala. Ikiwa kuna ufalme, hiyo ina maana kwamba kuna mfalme. Ufalme wa Mungu unamlenga Mfalme wetu mpendwa.

4. Tunaelewaje ufalme wa Mungu? Ushauri ni kwamba mahali pazuri pa kukuza uelewa wa ufalme wa Mungu ni kumtazama Yesu, Mfalme!

5. Tunataka kuzingatia mambo mawili ambayo Yesu anatusaidia kuelewa ufalme - kupitia Mifano na Maelezo yake.

   A. Mifano: Kwa kuonyesha mifano, tunamaanisha matendo, mambo ambayo Yesu alifanya ambayo yanatuonyesha jinsi ufalme wa Mungu unavyoonekana.

   B. Maelezo: Maelezo ni kuhusu maneno ambayo Yesu alitumia kutusaidia kuelewa ufalme. Yesu alitusaidia kuelewa ufalme kwa kusimulia hadithi kwenye umati na, wakati mwingine, kuzielezea kwa wanafunzi. Yesu alielezea ufalme kupitia mafundisho yake, na pia kupitia kuuliza na kujibu maswali.

6. Hebu tuangalie haya yote kwa undani zaidi, tukianza na Mifano. Hapa chini kuna baadhi ya kauli tunazoweza kutoa kuhusu ufalme wa Mungu, kulingana na matendo ya Yesu.

   A. Ufalme wa Mungu ni mahali ambapo wagonjwa huponywa.

B. Ufalme wa Mungu ni mahali ambapo wenye njaa hulishwa.

C. Ufalme wa Mungu ni mahali ambapo nguvu za giza hushindwa.

D. Ufalme wa Mungu ni mahali ambapo kila mtu ana thamani.

E. Ufalme wa Mungu ni mahali ambapo kila mtu anakaribishwa.

7. Kisha, hebu tuangalie Maelezo. Kuna sehemu kadhaa katika maandiko ambapo tunamsikia Yesu akisema, 'Ufalme wa Mungu ni kama ...' na kisha anasimulia hadithi ili kutusaidia kuelewa ufalme. Ni zipi baadhi ya hadithi za "ufalme wa Mungu ni kama ..." ambazo Yesu alisimulia?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓
✓

8. Ni njia gani zingine ambazo Yesu alitumia maneno kuelezea ufalme wa Mungu?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓
✓

9. Unaona uhusiano gani kati ya kuonyesha kwa vitendo na kuelezea ufalme wa Mungu?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓
✓
✓

10. Maisha ya Yesu yanatupa mfano wa jinsi ufalme unavyoonekana. Yanatupa mfano wa kufuata katika kuonyesha na kuelezea ufalme kwa wale wanaotuzunguka. Inaweza kuonekanaje kama tukifuata mfano wa Yesu leo?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓
✓

## Hadithi kutoka India

11. Hebu tuangalie mfano kutoka India.

*Miaka kumi au zaidi iliyopita nilitembelea kijiji kimoja nikifanya kazi na dhehebu maarufu la kiinjili la kimataifa na harakati za kimisionari. Kijiji hicho kilikuwa cha tabaka la chini na katika jimbo maskini sana la Kihindu lenye msimamo mkali.*

*Shirika liliendesha programu ya kikundi cha kujisaidia katika vijiji kama hivyo inayowezesha waumini wa kanisa hilo ambao walikuwa na mafunzo ya msingi katika kuanzisha vikundi vya kujisaidia vya wanawake. Walijulikana kama waandaaji wa maeneo. Lengo la vikundi hivi lilikuwa kuanzisha mfumo wa kuweka akiba ndogo ndogo na kutoa mikopo midogo midogo, kutoa muundo wa mafunzo katika ujuzi wa kujipatia riziki, na kukuza hatua za pamoja kushughulikia masuala ya kijamii, kiuchumi, kiroho, na kimazingira ambayo jamii yao inaweza kuwa inakabiliana nayo.*

*Katika kijiji fulani, waandaji wa maeneo walikuwa wakifanya maendeleo mazuri na kundi moja jipya lililowezeshwa ambalo lilikuwa limekabiliana na wamiliki wa ardhi wasio waadilifu ambao walitaka kuuza ardhi ya kijiji kwa mwekezaji. Hii isingewanyang'anya tu ardhi ya kilimo inayohitajika kutoka kwa wanakijiji lakini pia ingesababisha matatizo ya mazingira kutokana na uhaba wa maji na rasilimali chache za umwagilianji maji ya ardhini, uvujaji wa kemikali, na mmomonyoko wa udongo. Wamiliki wa ardhi walikuwa wakijaribu kuwagawanya wanakijiji kupitia mfumo usio sawa wa fidia.*

*Kikundi cha kujisaidia kilikuwa kikiweka akiba na kukopesha kwa mafanikio; wanawake kadhaa waliweza wameanzisha biashara ndogo ndogo au kuwasaidia waume zao kufanya hivyo. Waandaaji wa maeneo waliwasaidia wanawake kuanzisha mfuko wa akiba ndogo ndogo ili kusaidia kusimamia mwenendo usiokoma wa sikukuu za kidini. Uhusiano mkubwa wa kundi hili la wanawake ulikuwa ukianzishwa.*

*Siku moja, wanawake wa kikundi hicho walimuuliza muaandaji wa maeneo kama alikuwa ameolewa. Alijibu kwamba alikuwa ameolewa, nao wakamwuliza kwa nini hakupambwa kwa vito vya mke wa kitamaduni wa Kihindu. Alieleza kwamba, kama mfuasi wa Yesu, hakulazimika kupambwa kwa vitu hivyo vya tamaduni ya kihindu. Hili lilizua shauku kubwa. Wanawake hao waliuliza zaidi kuhusu imani yake na kama kulikuwa na kitabu kitakatifu ambacho wangeweza kukiona.*

*Katika ziara iliyofuata, alileta Biblia yake na, kwa kuwa wanawake hao hawakuwa na ujuzi wa kusoma na kuandika, akawasomea. Baada ya muda, wanawake wawili walimpa Yesu maisha yao. Katika imani za Kihindu za eneo hilo, wanawake waliokuwa wamejitoa kwa Yesu hawakuchukuliwa tena kuwa watu 'wao' na, ingawa bado walikuwa sehemu ya kundi hilo, walikabiliwa na mateso kutoka kwa majirani.*

*Siku moja, mtoto wa mwamini mmoja aliugua sana. Madaktari walisema mtoto huyo angekufa kama asipoongezewa damu. Kutokana na hali yao ya kuwa nje ya imani ya kihindu, majirani zao hawakuthubutu kuchangia damu kwa mtoto wao. Mwaandaji wa*

*maeneo iliitwa; alichangia damu na pia akamwomba Mungu juu ya uponyaji. Mtoto huyo alipona kimiujiza.*

*Mchanganyiko wa uponyaji wa kimiujiza na upendo wa waandaji wa maeneo uliwasukuma wengi zaidi katika jamii kumuelekea Yesu na leo kuna jamii kubwa ya wafuasi wa Yesu (VCJF) katika jamii hiyo.*

12. Ni njia gani maalum tunazoona ufalme wa Mungu ukionyeshwa na kuelezewa katika hadithi hii?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓
✓
✓

13. Tunaona ufalme wa Mungu ukitenda kazi juu ya mamlaka ya asili na ya kanuni za kimuujiza juu ya wamiliki wa ardhi, juu ya ugonjwa wa mtoto na juu ya mafundisho na imani ya Kihindu yaliyowakamata. Ufalme huo una alama ya uponyaji, ukombozi na ishara na maajabu mengine pamoja na maisha yaliyobadilika na utunzaji wa Mungu wa kila siku. Katika injili na Matendo tunaona kwamba wanafunzi walitenda haya, kama Wakristo wengi sana walivyofanya katika vizazi vyote. Je, tunatarajia Mungu kutenda hivi? Kama sivyo, hatutarajii au kuomba kwa ajili ya haya na kwa hivyo hatuna uwezekano mkubwa wa kupitia vipengele hivi vya ufalme wa Mungu.

14 Hatari ya kusoma hadithi fupi kama hii ni kwamba inasikika haraka, lakini kwa uhalisia, hadithi hii ilitokea kwa kipindi cha miaka miwili au mitatu. Tunapotafuta kuona ufalme ukiimarika katika jamii zetu, kwa kawaida hakuna suluhisho la haraka. Mabadiliko huchukua muda! Ni muhimu kukumbuka hilo ili tusivunjike moyo.

15. Kanuni ya Kwanza ni "Kuelewa Ufalme wa Mungu ni msingi".

A. Kama timu, kwa namna gani tunaweza kukuwa katika uelewa ufalme wa Mungu na unawezaje kuunda jinsi utakavyoingiliana na jamii?

B. Ni hali gani moja ambapo umekuwa ukitamani kuona ufalme wa Mungu ukija kwa nguvu ili kubadilisha?

16. Ni nini umejifunza kutokana na mjadala wa leo ambacho kimekuwa na maana kwako? Kwa nini?

17. Tafadhali chukua dakika chache wiki hii kujibu swali la tafakari ya kibinafsi lililo hapa chini. Utapata nafasi ya kushirikisha ulichoandika wiki ijayo.

Wanatheolojia wa Ufalme na wanafikra wa maendeleo huzungumzia kuhusu shalom au amani ya Mungu. Hili ni neno linalomaanisha mahusiano yaliyo sahihi, yaliyoponywa na yaliyorejeshwa katika viwango vingi. Bryant Meyers anasema:

> *Lengo la Mungu ni kuturejesha sisi na uumbaji wa Mungu katika utambulisho na kusudi letu la asili, kama watoto wanaoakisi sura ya Mungu. na kwa wito wetu wa asili kama mawakili wenye tija, wanaoishi pamoja katika mahusiano ya haki na amani. Malengo ya mabadiliko…ni malengo ya jamii na mwezeshaji wa maendeleo. (Kutembea na Maskini, Orbis, 2011 uk. 330)*

Ni kwa namna gani shalom ya uponyaji, mabadiliko na mafanikio inakuja katika maisha yangu mwenyewe?

Sura ya Kwanza, Ushahidi Usiogawanyika: Wafuasi wa Yesu, maendeleo ya jamii, na jamii ambazo hazijafikiwa na injili (Regnum 2020)



## Kanuni ya Pili: Kuelewa jinsi watu wanavyoingia katika ufalme wa Mungu hujenga jinsi tunavyofanya huduma.

Malengo ya Majadiliano Haya:

1. Kuaelewa vyema kwamba ingawa baadhi wanaweza kuashiria wakati maalum walipoamua kumfuata Yesu, kwa wengine ni mchakato unaotokea baada ya muda.
2. Tutagundua kwamba motisha wa kuingia katika ufalme wa Mungu ni tofauti kwa watu tofauti tofauti.
3. Tutakuwa na uelewa mpya wa umuhimu wa kuwapa watu uhuru wa kukubali au kukataa habari njema.

1. Wiki iliyopita tuliangalia Kanuni ya Kwanza: Kuelewa ufalme wa Mungu ni msingi. Tafakari ya kibinafsi ilikuwa kujibu: 'Ni kwa njia gani amani ya uponyaji, mabadiliko na mafanikio inakuja katika maisha yangu?'

2. Tuchukue dakika 3-4 kushirikishana jinsi tulivyojibu swali hilo.

3. Leo tutaangalia Kanuni ya Pili.

Muhtasari wa Kanuni ya Pili: *'Kuelewa jinsi watu wanavyoingia katika ufalme wa Mungu hujenga jinsi tunavyofanya huduma.'*

4. Watu huingiaje katika ufalme wa Mungu? Tunapoangalia Agano Jipya, tunaona kwamba hakuna jibu rahisi. Watu waliingia katika ufalme kwa njia tofauti tofauti.

   A. Kwa mfano, tumchukue Paulo. Paulo aliingiaje katika imani kwa Yesu?

   MAJIBU YAKO:
   ✓
   ✓
   ✓

   B. Baadhi ya watu, kama Paulo, wanaweza kuonyesha namna gani walivyopokea zawadi ya uzima wa milele.

   C. Vipi kuhusu Petro? Safari yake ya imani katika Yesu ilikuwaje?

   MAJIBU YAKO:
   ✓
   ✓
   ✓

D. Tunapomfikiria Petro, ni vigumu zaidi kubainisha jambo au tukio maalum wakati tunaweza kusema, alikuwa na imani ya kuokolewa katika Yesu. Hili ni kweli kwa watu wengi; safari yao ni mchakato wa hatua za polepole za kugeuka.

5. Vipi kuhusu wewe? Je, unaelezea safari yako imani kama tukio, au ilikuwa zaidi kama mchakato kwa muda fulani?

6. Jambo kuu ni kwamba hakuna ratiba ya mambo yote inayolingana kwa wote kwa wale wanaoingia katika ufalme wa Mbinguni. Wakati wa safari zetu ni tofauti.

7. Vivyo hivyo, nia yetu ya kuja kwenye imani labda pia ni tofauti.

8. Fikiria kuhusu safari yako ya imani. Ni nini kilichokuvutia kwenye injili? Ni nini kilichokuwa kizuri kuhusu habari njema, kwako?

9. Katika Maandiko, tunaona kwamba watu walimjia Yesu kwa sababu tofauti tofauti. Fikiria mifano kutoka katika Biblia. Ni zipi baadhi ya sababu zilizowafanya watu kuja kwa Yesu?

MAJIBU YAKO:

- ✓
- ✓
- ✓
- ✓

10. Watu wengi walimjia Yesu kwa sababu walikuwa na mahitaji ya dharura ambayo yeye pekee ndiye angeweza kuyatimiza. Alikidhi mahitaji yao bila kuweka masharti juu yao. Tunaweza kusema kwamba aliwapa watu uhuru wa kukubali au kukataa habari njema, na muda wa kufanya uamuzi.

11. Najiuliza kama tunatambua umuhimu wa kuwapa watu uhuru wa kukubali au kukataa habari njema kila wakati.

*Miaka kadhaa iliyopita Jawara (jina limebadilishwa) alianza kutembelea kanisa la David huko Uswisi. Jawara alikuwa mkimbizi Mwislamu ambaye alikuwa amewasili hivi*

*karibuni kutoka Afrika Magharibi. Watu wengi kanisani walimkaribisha kwa uchangamfu, wakimpa zawadi kama vile nguo za joto zilizosaidia kuzoea majira ya baridi kali. Ndani ya wiki chache tu, Jawara alimwambia mshiriki wa kanisa kwamba alikuwa amemwamini Yesu na alikusudia kubatizwa.*

*Na kisha, ghafla, Jawara alitoweka. Aliacha kuja kanisani. Hakuitikia simu za watu na aliepuka kuwasiliana na waumini wa kanisa. Baadaye David aligundua kwamba Jawara alikuwa amezoea starehe za msingi za maisha kama mtafuta hifadhi ambaye alikuwa amepewa hadhi ya ukimbizi na serikali ya Uswisi.*

*Watu wengi kanisani walijiuliza kama Jawara alikuwa ametumia mfumo huo. Je, alijipamba kwa sura ya kiroho ili kutumia ukarimu wao? Labda, lakini David alipendelea maelezo ya hisani zaidi.*

*Kama wakimbizi wengi nchini Uswisi, mambo ya misingi katika maisha yanatolewa na serikali. Lakini bado alihisi amepotea katika nchi hii mpya. Alikuwa amechanganyikiwa, mpweke, na mara nyingi alikuwa wabaridi. Watu kutoka kanisani walimkaribisha na kumsaidia kupunguza upweke. Walimpa vitu alivyohitaji na alihisi deni kwao. Mtu alipompa changamoto ya kumfuata Yesu, angewezaje kufanya chochote isipokuwa kuendelea?*

*Watu wa kanisani walikuwa na pesa, nguvu, na faida; kusema 'hapana' kwao ingewaletea aibu. Kwa hivyo Jawara alisema kwamba angemfuata Yesu. Moyo wake haukuwa katika uamuzi huo, na alijua kwamba marafiki zake wapya wangesikitishwa kwamba imani haikuwa ya dhati. Suluhisho lake pekee lilikuwa kuepuka kanisa kabisa.*

A. Unafikiri Jawara alihisi uhuru kiasi gani wa kukubali au kukataa habari njema?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

B. Kwa nini unafikiri ni muhimu watu wawe na uhuru wa kukubali au kukataa habari njema?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

12. Uelewa mzuri wa jinsi watu wanavyoingia katika ufalme wa Mungu unawezaje kuathiri jinsi timu yetu inavyofanya huduma?

13Tafadhali chukua dakika chache wiki hii kujibu swali la tafakari ya kibinafsi hapa chini. Utapata nafasi ya kushirikisha ulichoandika wiki ijayo.

## Kwa tafakari ya kibinafsi:

Ulipokuwa ukiingia katika imani katika Yesu Kristo, watu wengine walisema au walifanya nini kilichokusaidia? Walifanya nini kilichoweka vikwazo, au labda kilikusababisha kutoelewa habari njema?

Vipi kuhusu wale ambao wewe na timu yako mnataka waje kumjua Yesu? Ni mawazo gani kutoka kwa majadiliano haya yanayoathiri jinsi utakavyowakaribia katika siku zijazo?

## Kwa masomo zaidi...

*Sura ya Pili, Ushahidi Usiogawanyika*



# Kanuni ya Tatu: Injili huathiri mtu mzima (Kamaalivyo) na muktadha mzima.

Malengo ya Majadiliano Haya:

1. Timu yetu itaelewa vyema moyo wa Mungu kwa ajili ya mtu kama alivyo (mzima) na muktadha mzima wa watu.
2. Timu yetu itaelewa vyema jinsi dhamira kamili inavyoshughulikia mtu mzima na muktadha mzima wa watu.

1. Wiki iliyopita tuliangalia Kanuni ya Pili: Kuelewa jinsi watu wanavyoingia katika ufalme wa Mungu hujenga jinsi tunavyofanya huduma. Tafakari ya kibinafsi ilikuwa kuzingatia:

    Ulipokuwa ukiingia kwenye imani katika Yesu Kristo, watu wengine walisema au walifanya nini kilichokusaidia? Walifanya nini kilichoweka vikwazo, au labda kilikusababisha kutoelewa habari njema?

    Vipi kuhusu wale ambao wewe na timu yako mnataka wajekumjua Yesu? Ni mawazo gani kutokana na majadiliano haya yanayoathiri jinsi utakavyowakaribia katika siku zijazo?

2. Tuchukue dakika 3-4 kushirikisha jinsi tulivyojibu swali hilo.

3. Leo tunaangalia kanuni ya tatu.

Muhtasari wa Kanuni ya Tatu: *'Injili inaathiri mtu kama alivyo na muktadha mzima wa watu.'*

4. Kiini cha kanuni hii ni kwamba Mungu anatupenda kama viumbe vyake; amemuumba kila mmoja wetu kama kiumbe KAMILI.

5. Unawezaje "mtu mzima" mtu kama alivyo?

    MAJIBU YAKO:
    - ✓
    - ✓
    - ✓
    - ✓

    Mungu ametuumba tukiwa na mwili na roho. Tunapozungumzia mtu kamili, tunamaanisha ukweli kwamba kila mtu ameumbwa na zaidi ya kipengele kimoja. Mungu anajali miili yetu na roho zetu.

6. Ni wapi katika Maandiko unaona mifano mahususi kwamba Mungu anajali mwili, sehemu ya kimwili ya utu wetu? Jaribu kufikiria mifano kutoka Agano la Kale na Jipya.

MAJIBU AYKO:

✓
✓
✓
✓

7. Ni wapi katika maandiko tunaona kwamba Mungu anajali roho, sehemu ya kiroho ya utu wetu?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓
✓
✓

8. Tunaposema “Injili inamgusa mtu kama alivyo...” hii ni kwa sababu Mungu anamjali mtu mzima kamaalivyo.

9. Kanuni ya tatu inasema kwamba ‘injili inaathiri mtu mzima kama alivyo NA muktadha wote wa watu’. Tunaposema ‘muktadha’ tunarejelea si tu maeneo na maeneo bali pia masuala ya kijamii yaliyopo katika jamii anayoishi mtu huyo. Kwa mfano:

- Janga la VVU/UKIMWI
- Viwango vya juu vya uhalifu
- Umaskini
- Familia zisizo na utendaji kazi vizuri
- Biashara haramu ya binadamu

10. Unafikiri kwa nini ni muhimu kwamba injili inathiri muktadha mzima wa mtu?

- Injili inapoathiri muktadha mzima inaweza kufungua mlango kwa watu kutambua kwamba Mungu anajali.
- Injili inapoathiri muktadha wa mtu, ‘ufalme wa Mungu unakuja’ na ‘mapenzi yake yatatimizwa’

Sababu nyingine ni zipi?

✓
✓
✓

11. Rupen Das, mwanatheolojia wa Kanada na mfanyakazi mwenye uzoefu wa maendeleo ya jamii alisema:

*'Kinachowavutia maskini wengi ni Mungu anayeitikia, anae elewa mateso yao na yuko pamoja nao – Mungu anayejitambulisha kama Imanueli.' (Rupen Das)*

12. Yesu Kristo ni Bwana wa maisha yote na uumbaji, na sisi, tuliokombolewa kwake, ni mashahidi wake.

13. Hii inatuleta kwenye wazo la umisheni jumuishi. Unawezaje kufafanua neno 'jumuishi'?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓

14. Kwa hivyo tunapozungumzia kuhusu utume jumuishi (shahidi asiye gawantika), tunazungumzia kuhusu huduma inayoshughulikia mtu kama alivyo (mzima) na muktadha mzima wa watu.

Mwanatheolojia wa Ekuador Rene Padilla anasema kwamba 'utendaji wa utume kamili (usiogawanyika) unarudi kwa Yesu mwenyewe na kwa kanisa la karne ya kwanza.'

Yesu alitambua mahitaji ya kimwili ya wanadamu na aliyashughulikia. Pia alielewa kwamba uponyaji wa kimwili usingeshughulikia mahitaji ya ndani ya kiroho ambayo watu wanayo.

15. Hebu tuangalie kinachoweza kutokea ikiwa hatutatambua umuhimu wa kimwili na kiroho.

**A**. Je, ni hatari gani za huduma inayozingatia mambo ya kiroho pekee na kupuuza mahitaji ya kimwili ya watu?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓
✓
✓

**B.** Ni matatizo gani yanaweza kutokea ikiwa tutazingatia tu kukidhi mahitaji ya kimwili ya watu, lakini hatuhubiri au kufundisha kamwe?

MAJIBU YAKO:

- ✓
- ✓
- ✓

16. Tunaendeleaje, kama timu? Ni kwa njia gani huduma yetu huathiri mtu kwa ujumla wake (mzima) na muktadha mzima wa watu?

17. Tunaweza kufanya nini cha tofauti ili kufuata vyema mfano wa Yesu wa utume jumuishi (usiogawanyika)?

## Kwaajili ya tafakari binafsi:

Inamaanisha nini kwangu mimi binafsi kwamba Mungu anajali utu wangu 'mzima'?

Utimilifu wa 'mimi ni nani' unaonyeshwa katika jamii. 'Mimi ni nani' unaonyeshwaje katika jamii? (Timu, jamii ya wenyeji, n.k.)

## Kwa ajili ya kujifunza zaidi...

*Sura ya Tatu, Ushahidi Usiogawanyika*



# Kanuni ya Nne: Maono mapana ya kumtukuza Kristo

Malengo ya Majadiliano Haya:

1. Timu yetu itakuwa na uelewa mzuri zaidi wa maana ya kumtukuza Kristo.
2. Tutazingatia jinsi tunavyomtukuza Mungu tunaposhirikiana na kuhudumia jamii ambazo hazijafikiwa na injili na kuanza kutumia kile tunachojifunza katika huduma yetu.

## Mapitio

1.Wiki iliyopita tuliangalia Kanuni ya Tatu: Injili huathiri mtu kama alivyo (mzima) na muktadha mzima. Tafakari ya kibinafsi ilikuwa kuzingatia:

Inamaana gani kwangu mimi binafsi kwamba Mungu anajali utu wangu "wote"?

Utimilifu wa "mimi ni nani" unaonyeshwa katika jamii. "Mimi ni nani" unaonyeshwaje katika jamii? (Timu, jamii ya wenyeji, n.k.)

2. Tuchukue dakika 3-4 kushirikisha jinsi tulivyojibu swali hilo.

## Utangulizi

3. Wiki hii tutaangalia Kanuni ya Nne.

Muhtasari wa Kanuni ya Nne: *'Tunashirikisha maono mapana ya kumtukuza Kristo watu wanapoingia katika imani na jamii zinapoathiriwa na ufalme.'*

4. 'Kutukuza' ni neno tunalolisikia sana katika mazingira ya Kikristo. Lakini inamaanisha nini kumtukuza mtu? Hebu tujadili.

Fikiria kuhusu neno kama linavyotumika katika Biblia. Ukiweza, chukua muda kutafuta neno 'kutukuza' kwenye simu yako au kompyuta au kamusi ikiwa una moja karibu.

5. Uligundua nini?

MAJIBU YAKO:
- ✓
- ✓
- ✓
- ✓

6. Je, fafanuzi hizi zinakupa ufahamu gani kuhusu maana yako binafsi kumtukuza Mungu?

MAJIBU YAKO:
- ✓
- ✓
- ✓
- ✓

7. Yesu alimtukuza Mungu, si tu kwa mambo aliyofanya na aliyosema, bali pia kwa jinsi alivyo. Utu wake na tabia yake vilimtukuza Mungu vilipoingiliana kwa upendo na watu na katika urafiki alioujenga.

8. Tuache kufikiria mambo tunayofanya ambayo humletea Mungu utukufu na tufikirie kuhusu 'uwepo' sehemu ya maisha yetu: mioyo yetu, tabia zetu na mtazamo wetu. Kwa mfano, Yesu alikuwa mvumilivu sana kwa wanafunzi wake. Hilo lilimtukuza Mungu kwa sababu liliwakilisha tabia yake kwa njia ya kweli.

9. Ni mitazamo au sifa gani zingine ambazo tunaweza kuwa nazo, au tunatamani kuwa nazo, zinazowakilisha moyo wa Mungu?

MAJIBU YAKO:
- ✓
- ✓
- ✓
- ✓
- ✓
- ✓

10. Fikiria jinsi Yesu alivyowajibu watu waliokuwa na uhitaji. Injili inatuambia nini kilimsukuma kufanya hivyo?

MAJIBU YAKO:
- ✓
- ✓
- ✓
- ✓
- ✓

11. Fikiria njia ambazo wewe, timu yako, na kanisa lako mnavyowajibu watu wenye uhitaji.

**A.** Ni zipi baadhi ya njia wanazotumia kujibu?

MAJIBU YAKO:

✓
✓

**B.** Unafikiri nia yako ni ipi? Yaani, unatumaini nini kitokee kama matokeo?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓
✓
✓
✓

**C.** Je, utaendelea kuwajibu watu wenye uhitaji kwa njia hizi hata kama unajua kwamba wachache, kama wapo, watakuwa wafuasi wa Yesu? Kwa nini, au kwa nini usifanye hivyo? Fikiria kuhusu yale uliyofanya hapo awali na pia kuhusu Yesu alimlisha nani, alimponya na kumsaidia.

**D.** Nia hizi zinasaidiaje kumtukuza Mungu? Je, zinafanyaje kinyume chake?

## Hitimisho

12. Hebu tufikirie kuhusu Yesu.

*'Mwana ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote.' Wakolosai 1:15*

13. Yesu alikuja kumwakilisha Mungu, kuwasaidia watu kuona picha halisi ya yeye ni nani. Sasa sisi ndio tunaomwakilisha, tunauakisi utukufu wa Mungu kwa wale wanaotuzunguka. Tunapobadilishwa, tunamuakisi Yesu. Hatufanyi hivyo kwa nguvu zetu wenyewe, kama vile mwezi usivyong'aa wenyewe, unaakisi jua.

*'Na sisi sote, ambao kwa nyuso zisizofunikwa tunaakisi utukufu wa Bwana, tunabadilishwa tufanane naye kwa utukufu unaozidi kuongezeka, unaotoka kwa Bwana, aliye Roho.' (2 Wakorintho 3:18)*

14. Ni nini kimekuwa na maana kwako katika mjadala huu?

## Kwa ajili ya kutafakari kibinafsi:

Tabia ya Mungu inaonekanaje katika maisha ya watu unaowajua? Je, unaweza kufikiria kumtia moyo mmoja (au zaidi) kwa kushiriki jinsi unavyoona tabia ya Mungu inavyoonekana katika maisha yao?

Utukufu wa Mungu unaonekanaje kupitia timu yangu? Je, tunaisaidia jamii yetu na wale tunaowahudumia kuona tabia ya Mungu?

## Kwa masomo zaidi...

Sura ya Nne, Ushahidi Usiogawanyika



# Kanuni ya Tano: Maombi, vita vya kiroho na mabadiliko

Malengo ya Majadiliano Haya:

1. Timu itakua katika uwezo wa kutambua vita vya kiroho.
2. Kuwa na ujasiri katika ukweli kwamba hatuna cha kuogopa.
3. Timu yetu itatambua zana maalum tutakazotumia katika kukabiliana na vita vya kiroho.

1. Wiki iliyopita tuliangalia Kanuni ya Nne: Maono mapana ya kumtukuza Kristo. Tafakari ya kibinafsi ilikuwa kuzingatia:

    Tabia ya Mungu inaonekanaje katika maisha ya watu unaowajua? Je, unaweza kufikiria kumtia moyo mmoja (au zaidi) kwa kushirikisha jinsi unavyoona tabia ya Mungu inavyoonekana katika maisha yao?

    Utukufu wa Mungu unaonekanaje kupitia timu yangu? Je, tunasaidia jamii yetu na wale tunaowahudumia kuona tabia ya Mungu?

2. Tuchukue dakika 3-4 kushirikisha jinsi tulivyojibu swali hilo.

3. Wiki hii tutaangalia Kanuni ya Tano.

Muhtasari wa Kanuni ya Tano: *'Maombi na vita vya kiroho ni sehemu muhimu za mchakato wa mabadiliko'*

4. *Tunapofikiria kuhusu 'vita vya kiroho' kuna uwezekano kwamba mambo tofauti yanakuja akilini mwetu, na hasa ikiwa sisi ni sehemu ya timu ya kimataifa. Tuanze na maombi, kuomba hekima na utambuzi tunapoingia katika mjadala huu muhimu.*

## Vipengele Tofauti vya Vita vya Kiroho

5. Vita vya kiroho na maombi ni sehemu muhimu ya maendeleo ya jamii. Wazo kuu la vita vya kiroho ni kwamba tuna adui anayetaka kututenganisha na Mungu. Hajali jinsi anavyofanya.

    Mwandishi wa sura ya 5 katika kitabu cha mashahidi wasiogawanyika aliandika:

    *Tunaweza kufikiria majeraha makubwa na ajali kama mashambulizi ya kiroho. Labda tunafikiria mila na laana za kishetani. Mara chache sana, tunafikiria mapambano dhidi ya miundo mbovu ya nguvu na nguvu ya ushawishi ya udanganyifu inayoendelea kuwaponda watu na kuwaweka mbali na Mungu.*

Leo tutazingatia mikakati mitatu ambayo adui hutumia: uchawi wa wazi, miundo mbovu ya nguvu, na maisha ya kila siku.

Kulingana na ukubwa wa kikundi chetu cha masomo na udhabiti wa mtandao kwa mafunzo ya mtandaoni, tunaweza kugawanyika katika makundi matatu.Tukigawanyika, kila kikundi kitazingatia kipengele tofauti na kutoa ripoti kwa kikundi kizima.

**A**. Kundi la kwanza litaangalia uchawi wa waziwazi, sehemu ya kwanza chini.

**B.** Kundi la pili litaangalia miundo mibovu ya nguvu (uovu wa kimfumo), sehemu ya pili chini.
**C**. Kundi la tatu litaangalia masuala ya maisha ya kila siku, sehemu ya tatu chini.

Tutakuwa na dakika kumi katika vikundi vyetu vya kujadiliana. Kila kikundi kinapaswa kuwa na mtu anayeandika maarifa mawili au matatu muhimu na kuwa tayari kushirikisha makundi mengine tutakaporudi pamoja.

Hakikisha unazungumzia jinsi mabadiliko yalivyotokea katika kila moja ya hadithi hizi.

## Kikundi cha Kwanza: Uchawi Mbaya

Soma hadithi ifuatayo kwa pamoja:

*Mnamo mwaka 2006, wafanyakazi wetu wa kwanza walipohamia mpaka wa Zambia kwenye ufukwe wa ziwa Tanganyika, walisikia kuhusu sifa ya eneo hilo kwa nguvu za giza za kiroho: dhabihu za damu za wanadamu na wanyama zilikuwa msingi wa mila zilizofanywa kwa vizazi vingi. Nilipojiunga nao mwaka wa 2008, niligundua kwamba kazi nyingi za timu zilikuwa, kwa busara, kujenga msingi wa kiroho.*

*Tulikumbwa na ukosefu wa chakula, mavazi, huduma ya msingi katika afya, na elimu katika jamii hizi. Hatimaye, mbinu yetu ilijumuisha afya, elimu, na kufundisha kuhusu matumizi bora ya maliasili. Lakini ilikuwa dhahiri kwamba mabadiliko yalipaswa kutokea kwanza ndani ya msingi wao wa kiroho. Katika kijiji kimoja, mmarekani alijenga shule na kliniki. Alituambia kuchanganyikiwa kwake kwamba, licha ya uwekezaji mkubwa katika jamii, tabia za uharibifu za watu hazikubadilika.*

*Mabadiliko ya kudumu yanatokeaje? Timu yetu ilikuwa imeanza na ukweli mkuu kwamba upendo mkamilifu huondoa hofu (1 Yohana 4:18). Tukitambua kwamba vita vyetu si juu ya mwili na damu (Efe. 6:12), na badala ya kuzingatia shughuli hizo muhimu za afya na ustawi, timu yetu ilikipa kipaumbele maombi ya matembezi na kutangaza maandiko. Siku tatu kwa wiki, tulitembea katika vijiji kuanzia saa 12 asubuhi hadi 1 asubuhi, tukisoma mistari ya biblia kwa sauti. Nidhamu hii ya uaminifu ilikuwa tofauti inayoonekana na thabiti na desturi za kawaida za jamii.*

*Tuliona kwamba uwepo hai wa Roho Mtakatifu ulizidishwa katika maeneo haya ambapo imani ya watu katika mambo ya ajabu ilikuwa tayari imara. Walihitaji tu kubadilisha imani yao kutoka kutarajia kwamba laana ingewafanya wawe wagonjwa au wenye njaa hadi kuamini kwamba Mungu muumba anataka kuwaponya. Wengi waliponywa na kukombolewa kupitia maombi. Watu walianza kuona wazi kabisa kuchagua kati ya imani katika Mungu na mila za waganga, kama ilivyotokea katika kijiji ambapo mke wa mkuu wa shule alikuwa mganga lakini alichagua kumwamini Mungu, kuonyeshwa kwa nguvu ya Yesu ya ukombozi.*

*Katika kijiji hicho Gloria**, mke wa mvuvi wa kijiji, alikuja kwa Alfred*, mmoja wa timu yetu, kwa sababu ya mimba nyingi zilizoharibika. Katika kila ujauzito wake uliopita, aliota kisu kikimshambulia na anapoteza mtoto siku inayofuata. Alipofika kwa Alfred, mwanamke huyo alikuwa mjamzito tena; alimsihi amwombee mtoto mwenye afya njema. Siku moja baada ya hapo, Gloria alimjia Alfred akiwa na huzuni kwa sababu alikuwa ameota tena kuhusu shambulio la kisu. Alfred alimwombea Gloria, ambaye baadaye alijifungua mtoto wake wa kwanza mwenye afya njema. Baadaye, Alfred mwenyewe aliota ndoto ya kusumbua ya kisu kikimshambulia, lakini aliamka, akamkemea pepo huyo kwa jina la Yesu, akacheka jaribio la adui la kumtisha, na akaendelea kulala kwa amani.*

## Maswali ya majadiliano:

**A.** Unaona wapi ushahidi wa aina ya uchawi dhahiri wa vita vya kiroho katika hadithi hii?

**B.** Washiriki wa timu waliingiaje wakiwa wamekingwa kikamilifu na silaha za Mungu?

**C**. Uwepo wa timu katika jamii ulionyeshaje ufalme wa Mungu?

**D.** Ni mabadiliko ya aina gani yaliyotokea?

## kundi la Pili: Miundo ya mamlaka Iliyoharibika (da

Tunapozungumzia uovu wa kimfumo, tunarejelea mambo kama....

- Watu na mamlaka wanaowezesha biashara haramu ya binadamu
- Sheria na watu wenye nguvu wanaowaweka wengine katika umaskini na kazi za mishahara midogo
- Makampuni yaliyounganishwa na wanasiasa na maafisa wa serikali ili kuwawezesha kuepuka kanuni za uchafuzi wa mazingira
- Polisi, maafisa wa forodha na uhamiaji wanaotoza faini au hawafanyi wanachopaswa kufanya bila kupewa rushwa.

Tusome hadithi ifuatayo pamoja:

*Hope* alipelekwa Ugiriki kutoka nchi yake alipokuwa mdogo sana na kulazimishwa kuingia katika biashara ya ngono. Baada ya kukutana na Rosie na timu yake, na kuzungumza naye, Hope aliamini kuwa ilikuwa njia mbaya ya kuishi na alitaka kuiacha. Hata hivyo, haikuwa rahisi sana.*

*Hope alikuwa amekuja Ugiriki bila hati rasmi za utambulisho, kwa hivyo kazi yote aliyoweza kupata ilikuwa kinyume cha sheria na inalipwa vibaya. Hope aliishia kufanya kazi katika hoteli na jikoni katika misimu ya watalii kwa mshahara mdogo, akijaribu kuwaepuka waajiri waliodhani walikuwa na haki ya 'huduma' zingine kutoka kwa msichana mrembo wa kuosha vyombo.*

*Ingawa Hope alivumilia na akafanikiwa kupata kazi nje ya biashara ya ngono, imemtia alama kisaikolojia. Hata miaka michache baadaye, Hope aliteseka kumwamini mtu yeyote, na alipendelea kazi ambapo sio lazima awe sehemu ya kukutana na watu. Alitegemea kutendewa vibaya na watu hao. Rosie na timu yake walizungumzia juu ya msamaha, lakini haikuleta maana kwake katika maisha yake mwenyewe. Ingawa Hope anaamini katika Mungu, bado hakupata neema binafsi ya kuelewa inaweza kumaanisha nini kwake.*

*Mungu amekuwa halisi katika maisha ya Hope, alisema Rosie. 'Lakini kuna wanawake wengi zaidi bado wanafanya kazi katika madanguro na katika mitaa ya Ugiriki. Wana haki sawa ya kumjua na kujifunza kumwamini Mungu anayeokoa na kulinda, na kujifunza kujithamini kama vito vya thamani, jambo ambalo linaanza kutokea wakati Rosie ikiwa na maono ya uhasilia ya kuanzisha kampuni isiyo ya faida, kutoa njia mbadala ya kufanya kazi kwa afya kwa wanawake walio hatarini nchini Ugiriki.*

*Jina la Hope limebadilishwa ili kuheshimu faragha yake. Hadithi imechukuliwa kutoka ‘Tumaini la matumaini huko Ugiriki’, kutoka OM Communications.

## Maswali ya majadiliano

**A**. Unaona wapi ushahidi wa mfumo wa mamlaka ulioharibika katika hadithi hii?

B. Ni kwanjia gani timu ilipingana na mfumo wa mamlaka ulioharibika? Walishiriki vipi katika vita vya kiroho zaidi ya maombi, kufunga au kuabudu?

**C.** Uwepo wa waamini katika jamii ulifunuaje ufalme wa Mungu?

**D**. Ni mabadiliko ya aina gani yaliyotokea?

## Kikundi cha tatu: Maisha ya kila siku

Tusome hadithi zifuatazo pamoja:

Hadithi ya Johanna, kutoka sura ya 5 katika Ushahidi Usiogawanyika:

*Upinzani wa kiroho unaweza kuja katika hali ngumu ya maisha ya kila siku. Mwenzangu huko Asia aliandika: Tunahisi kwamba upinzani wa kiroho unakuja kama mawimbi, na mara nyingi kwa njia ambazo hatutarajii. Hatujapata upinzani kutoka kwa taasisi za kidini au serikali za mitaa, ambao kwa kweli wamezikaribisha kazi yetu kwa sababu wanaona faida zinazoonekana kwa watoto na familia tunazofanya kazi nazo. Lakini naona inakuja kwa njia fiche katika timu yetu ya maendeleo ya jamii, kupitia kukata tamaa, kutoelewana*

*na migogoro, magonjwa, masuala ya visa, na kukatishwa tamaa kwingine, ambayo nahisi inataka kutujia "kutokea ndani"*

Hadithi ya Rebecca

*Rebecca alikuwa ameketi mbele ya kompyuta yake, akijaribu kuandaa warsha ambazo yeye na timu wataongoza wiki ijayo barani Afrika. Atasafiri hivi karibuni kwenda kwenye tukio hilo, lakini kwa siku kadhaa kila aina ya usumbufu uliendelea kujitokeza. Alikuwa akizidi kuchanganyikiwa na kukasirika kadri changamoto zilivyomzuia kuzingatia maandalizi. Aliinuka kutoka kwenye kompyuta yake na kuingia kwenye korido yenye zulia. Alipofanya hivyo, alisikia 'mlio' mkubwa chini ya mguu wake. Alitazama chini na hakika korido ilikuwa imejaa maji kabisa. Ilibainika kuwa tanki lake la maji taka lilikuwa limejaa maji, na kupeleka maji machafu bafuni, korido na chumbani kwake. Ilikuwa wakati huo ndipo alipogundua kuwa vikengeushio na kukatishwa tamaa katika siku zilizopita havikuwa vitu vya nasibu/bahatimbaya tu. 'Lazima Mungu anampango wa kufanya jambo kubwa wakati wa mafunzo haya ikiwa adui anafanya kazi kwa bidii kunivuruga!' Mara tu alipotambua mkakati wa adui, mtazamo wake ulibadilika. Alianza kuvuta zulia lenye maji kwa moyo wa furaha na kuendelea kujiandaa akiwa na uhakika kwamba Mungu alikuwa na mipango mikubwa kuliko alivyokuwa akifikiria.*

## Maswali ya majadiliano

A. Kutokana na hadithi zilizo hapo juu, ni mifano gani maalum ya upinzani wa kiroho katika matukio ya kawaida ya maisha ya kila siku?

B. Tulisema hapo awali kwamba adui hutumia vita vya kiroho kututenganisha na Mungu. Je, aina za vitu ambavyo tumeorodhesha zinawezaje kututenganisha na Mungu na kusudi lake kwa maisha yetu?

C. Umepitiaje vita vya kiroho katika matukio ya kawaida ya maisha ya kila siku?

D. Ni mabadiliko gani yalitokea?

6. Tusikie kutoka kwa kila kikundi. Kila kikundi kitashirikisha kuhusu aina ya vita vya kiroho walivyoangalia na jambo moja au mawili muhimu kutoka kwa majadiliano, ikiwa ni pamoja na ushahidi wa mabadiliko yaliyotokea.
7. Jambo la pili tunalotaka kulizingatia ni ukweli kwamba hakuna cha kuogopa.

Holly Steward anaandika katika Mashahidi Wasiogawanyika:

> *'Katika uzoefu wangu nchini Zambia, ishara ya kwanza ya jamii iliyofungwa na adui ni hofu; kwingineko inaweza kuonekana katika kukata tamaa, uchoyo, vurugu, au ubinafsi.'*
>
> Katika muktadha wa timu yetu, ni zipi zinaweza kuwa baadhi ya ishara za jamii iliyofungwa na adui?
>
> Ni nini inaweza kuwa ishara za mabadiliko, kwamba utumwa unavunjika?

Holly Steward anaendelea katika sura inayofuata katika kitabu cha Mashahidi Wasiogawanyika:

*Wengi wa wanachama wa timu yetu walikuwa Wazambia wenye ujuzi na elimu ndogo. Katika kijiji kimoja kwenye ziwa tanganyika, tuligundua kwamba mkuu wa kijiji—ambaye pia alikuwa mganga wa kienyeji—aliona kitu ziada ndani yao. 'Roho aliye pamoja nanyi ana nguvu zaidi kuliko ile tuliyonayo ndani yetu,' aliwaambia. 'Hirizi na mila zetu hazifanyi kazi tena sasa kwa kuwa Roho aliye ndani yenu yuko katika kijiji chetu.*

8. Maandiko yanatuambia kwamba 'upendo kamili huondoa hofu' (1 Yohana 4:18). Unajibuje wazo la upendo kamili kuondoa hofu, katika muktadha wa vita vya kiroho?

9. *Holly pia aliandika: 'Shukrani kwa Yesu, tuko upande wa ushindi wa vita hivi ambavyo tayari tumevishinda! Hata kama mashambulizi ya kiroho yanaleta fumbo au wasiwasi, sisi ni "zaidi ya washindi" (Rum 8:37), si tu kwamba tunalindwa bali pia ni wapiganaji hodari ambao uovu lazima ukimbie.'*

## Ni zana au mbinu zipi tunaweza kutumia?

10. Kuwa na ufanisi kunahusisha zaidi ya kutambua vita vya kiroho na kutoogopa. Mungu ametupa zana maalum ambazo tunaweza kuzitumia tunapoingia katika vita vya kiroho. Mazoea matatu muhimu ni:

    A. Kutangaza neno la Mungu: Maandiko yana athari kubwa katika anga la kiroho kwa sababu neno la Mungu lina nguvu. Li hai na lina nguvu, lina ukali kuliko upanga wenye makali kuwili (Ebr. 4:12). Ni ukweli gani ambao timu yetu itatangaza? Tutafanya kwa namna gani?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

B. Kufurahi: Kufurahi kulikuwa sehemu gani katika vita vya kiroho kwenye maandiko haya? Inawezaje kuwa sehemu ya kile wewe na timu yako mnakifanya kwa kusudi?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

C. Kutubu: Kutubu kunawezaje kuwa sehemu ya jinsi unavyoshiriki katika vita vya kiroho? (Tazama Danieli 9:4-6.)

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

11. Tunawezaje kukusanya pamoja yale tuliyojifunza kuhusu vita vya kiroho?

Walter Wink (katika Kutaja mamlaka) alisema kwamba:

*Lazima tujenge usikivu mzuri kwa kile ambacho wazee walikiita 'vita mbinguni.' ... Wito wa kipekee wa kanisa katika mabadiliko ya kijamii upo katika kuweka wazi asili mbili ya kazi yetu. Tunapigana katika pande mbili, ya duniani na ya mbinguni.*

Tukitaka kuona mabadiliko, kuona jamii zenye hamasa kweli katika kumjua Kristo, na katika jamii maalum za wafuasi wa Yesu, jambo hilo litatokeaje?

Tunapaswaje, na kwa zana gani (au mbinu au silaha) kushiriki katika vita vya kiroho ili mabadiliko hayo yaweze kutokea?

*'Mwana ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote.' Wakolosai 1:15*

## Kwa ajili ya kutafakari kibinafsi:

Ni nini kimekuwa muhimu kwako katika mjadala wa leo kuhusu vita vya kiroho? Je, imekuwa ni kutafakari zaidi mambo ambayo tayari unayajua na umeyapitia, au umejifunza kitu kipya? Kwa msaada wa Mungu, unawezaje kutumia mawazo haya katika vitendo?

## Kwa masomo zaidi...

*Sura ya Tano, Ushahidi Usigawanyika.*



# Kanuni ya Sita: Kutunza uumbaji kama ibada, ushuhuda na utii

Malengo ya Majadiliano Haya:

1. Timu itakuwa na uelewa wa kina wa maana ya kutunza uumbaji na kwa nini ni muhimu kama kitendo cha ibada na utii na kama ushuhuda kwa wale wanaotuzunguka.
2. Kutunza uumbaji ni thamani inayoonyesha sisi ni nani na jinsi tunavyoishi, na si tu kama shughuli au programu tunayoongeza kwenye mambo mengine.

## Mapitio

1. *Wiki iliyopita tuliangalia Kanuni ya Tano: 'Maombi na vita vya kiroho ni sehemu muhimu za mchakato wa mabadiliko'*

2. Tafakari ya kibinafsi ilikuwa kuzingatia kile ambacho tayari ulikuwa unakijua na kile ulichojifunza kuhusu vita vya kiroho. Je, kulikuwa na mambo ambayo ungependa kuyaweka katika vitendo, kwa msaada wa Mungu?

   Tuchukue dakika 3-4 kushirikisha jinsi tulivyojibu maswali hayo.

## Utangulizi

3. Wiki hii tutaangalia Kanuni ya Sita.

Muhtasari wa Kanuni ya Sita: *'Kutunza uumbaji ni usemi wa ibada, ushuhuda na utii.'*

4. Tunaona nini kinachotuzunguka na katika jamii yetu kinachoonyesha maajabu ambayo Muumba wetu aliweka katika mazingira tunayoishi?

   MAJIBU YAKO:
   ✓
   ✓
   ✓

5. Nini kinachoonyesha uharibifu kwa ulimwengu ambao Mungu aliumba?

   MAJIBU YAKO:
   ✓
   ✓
   ✓

6. Ni nini kinachokuja akilini unaposikia maneno 'kutunza uumbaji'?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

7. Ni kwa njia gani kutunza uumbaji ni tendo la ibada kwa Mungu?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

8. Inawaeleza nini wale wanaotuzunguka, wakati Wakristo wanaonekana kutojali kuhusu kutunza dunia?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

9. Kutunza uumbaji kunawezaje kuwa ushuhuda kwa wale wanaotuzunguka?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

10. Kanuni hii inasema kwamba kutunza uumbaji pia ni kitendo cha utii. Ni wapi katika maandiko tunaagizwa kutunza uumbaji?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

## Kuangalia maandiko

11. Maandiko yanasema nini kuhusu kutunza uumbaji? Hebu tusikilize mahojiano mafupi na Dkt. Robert Sluka, mwanabiolojia wa baharini anayefanya kazi na A Rocha, shirika la Kikristo la kimataifa linalolenga kutunza uumbaji. Bob na familia yake waliishi kwa miaka kadhaa Asia Kusini na sasa anasaidia nchi mbalimbali kote ulimwenguni.

KUMBUKA: Ikiwa video ya mahojiano haipatikani, tafadhali nenda kwenye vifungu vya maandiko na maswali mwishoni mwa kitengo hiki, kisha urudi kwenye swali la 11 utakapokamilisha sehemu hiyo.

VIDEO INAPATIKANA KWA KUBONYEZA KIUNGO HIKI:
https://vimeo.com/605038367/82bee419db

12. Dkt. Sluka alisema nini kuhusu uzoefu wake mwenyewe ambao ulikuvutia?

Je, alisema chochote kuhusu Yesu na kuhusu uumbaji ambacho kilikuwa kipya kwako?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

Dkt. Sluka alizungumzia kuhusu kaa mdogo, na kwamba kaa katika 'uovu wake wote' ni sehemu ya ibada ya Mungu duniani. Hiyo ina maana gani? Uumbaji unamsifuje Mungu?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

Je, mawazo ambayo Dkt. Sluka amewasilisha yanakupatia changamoto gani, au yanakutia moyo vipi, unapofikiria kuhusu kutunza uumbaji?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

## Kwa namna gani tutaweza ...

13. Tulianza mjadala wetu leo kwa kutazama maajabu ambayo muumba ameweka karibu nasi. Kisha tukaangalia uharibifu ambao umefanywa kwa uumbaji.

Jamii ya wafuasi wa Yesu yenye nguvu kweli inaweza kufanya nini ili kuhifadhi uzuri na kurekebisha uharibifu?

Kwa namna gani kutunza uumbaji kunaweza kuchangia katika uundaji wa jamii zenye nguvu za wafuasi wa Yesu?

MAJIBU YAKO:

- ✓
- ✓
- ✓

## Hitimisho

14. Kutakuwa na tofauti gani ikiwa tutafikiria kutunza uumbaji kama thamani inayoathiri jinsi tunavyoishi na tunachofanya (kama vile uadilifu, wema, au kuwaheshimu watu wengine) badala ya kufikiria kama shughuli au programu tunayotekeleza?

15. Ni hatua gani moja ambayo sisi, kama timu, tutachukua ili kutunza vyema uumbaji?

## Kwa ajili ya kutafakari kibinafsi:

Fikiria kuhusu jamii ambayo haijafikiwa na injili ambayo unaihudumia au kuiombea. Wanapojifunza kumhusu na kuanza kumgeukia Yesu, wanawezaje kujifunza kwamba kutunza uumbaji ni sehemu ya kuwa mfuasi wa Yesu?

## Kwa masomo zaidi…

*Sura ya Sita, Ushahidi Usiogawanyika.*

Au tazama video fupi kumi na mbili kuhusu utunzaji wa uumbaji kutoka Darasa la Kimataifa la Lausanne katika: https://www.lausanne.org/lausanne-global-classroom/creation-care-episode

## Kwa wale ambao hawakuweza kutazama video hiyo na Dkt. Robert Sluka

Tafakari vifungu vifuatavyo:

*Wakolosai 1:15-20*
*Mwana ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. 16 Kwa maana katika yeye vitu vyote viliumbwa: vilivyo mbinguni na vilivyo duniani, vinavyoonekana na visivyoonekana, ikiwa ni viti vya enzi au mamlaka au watawala au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kupitia yeye na kwa ajili yake. 17 Yeye alikuwako kabla ya vitu vyote, na katika yeye vitu vyote vinashikamana. 18 Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani kanisa; yeye ndiye mwanzo na mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu, ili katika kila kitu awe mkuu. 19 Kwa maana Mungu alipenda utimilifu wake wote ukae ndani yake, 20 na kwa njia yake apate kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake, ikiwa ni vitu vilivyo duniani au vilivyo mbinguni, kwa kufanya amani kwa damu yake, iliyomwagika msalabani.*

Jambo kuu mmoja kutoka kwa kifungu hiki ni kwamba kuna uhusiano wa aina tatu Yesu anao na uumbaji, si jukumu kubwa (kama kuwa mzaliwa wa kwanza) bali kitu alichofanya, anachofanya, au atakachofanya. Je, unaweza kuona majukumu hayo matatu?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

Viumbe vyote mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Viumbe humwabuduje Mungu?

*Ufunuo 5:9-13*
*9 Nao wakaimba wimbo mpya, wakisema, "Unastahili kukitwaa kitabu na kufungua mihuri yake, kwa sababu ulichinjwa, na kwa damu yako ukamnunulia Mungu watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa. 10 Umewafanya kuwa ufalme na makuhani wamtumikie Mungu wetu, nao watatawala [a] duniani." 11 Kisha nikatazama nikasikia sauti ya malaika wengi, idadi yao ikiwa elfu nyingi, na elfu kumi mara elfu kumi. Wakakizunguka kiti cha enzi na wale viumbe hai na wazee. 12 Kwa sauti kubwa wakasema,*
*"Anastahili Mwana-Kondoo, aliyechinjwa, kupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na sifa!"*

*13 Kisha nikasikia kila kiumbe mbinguni na duniani na chini ya nchi na juu ya bahari, na vyote vilivyomo, vikisema: "Kwake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi na kwa Mwana-Kondoo iwe sifa na heshima na utukufu na nguvu, milele na milele!"*

*Chunguza kwa makini kifungu hiki. Ni nani anayemsifu Mungu na Mwanakondoo?*

Je, haya ni mawazo mapya kwako kuhusu Yesu na uumbaji?

Wanawezaje kuleta mabadiliko, kukupa changamoto au kukuhimiza, unapofikiria kutunza uumbaji?

Sasa rudi kwenye Swali la 11 hapo juu.



# Kanuni ya Saba: Maono kwa jamii za watu walio mpkea Yesu na upya wa watu binafsi na jamii.

Malengo ya majadiliano haya:

1. Watu katika timu watatambua umuhimu wa kuwasikiliza wengine, hasa wafuasi wa Yesu miongoni mwa jamii tunayoihudumia.
2. Watu katika timu wataona umuhimu wa kuwa na maono wazi kwa ajili ya uundaji wa jamii za wafuasi wa Yesu.
3. Watu katika timu wataona uhusiano kati ya wakati, nia, na kuonyesha na kuelezea habari njema.

## Mapitio

1. 'Wiki iliyopita tuliangalia Kanuni ya Sita: 'Kutunza uumbaji ni kufanya ibada, ushuhuda na utii.'

2. Tafakari ya kibinafsi ilikuwa kufikiria kuhusu jamii ambayo unaihudumia au kuiombea ambayo haijafikiwa na injili. Wanapojifunza kumhusu na kuanza kumgeukia Yesu, wanawezaje kujifunza kwamba kutunza uumbaji ni sehemu ya kuwa mfuasi wa Yesu?

   Tuchukue dakika 3-4 kushirikisha jinsi tulivyojibu maswali hayo.

## Utangulizi

3. Wiki hii tutaangalia Kanuni ya Saba.

*Muhtasari wa Kanuni ya Saba: 'Mabadiliko ya kweli yanahitaji maono kwa jamii zenye hamasa yakuwa wafuasi wa Yesu na upya wa watu binafsi na jumuiya.'*

4. Unaweza kuelezeaje neno 'upya'?

   MAJIBU YAKO:

5. Hebu tufikirie hadithi ili kuonyesha jinsi 'maono ya upya na jamii yenye msukumo wakuwa wafusai wa Yesu' inavyoonekana.

> *Mwanzoni mwa miaka ya 2000, mashirika mawili ya kimisheni ya Kikristo yalianza kufanya kazi katika sehemu ya mbali ya nchi huko Asia. Kazi yao ililenga afya na maendeleo ya jamii na elimu isiyo rasmi. Wajumbe wa timu, Wakristo na wasio Wakristo, walifanya kazi pamoja na wanajamii na kwa miaka kadhaa waliona maboresho makubwa katika afya ya wanawake na watoto, maji na usafi wa mazingira, usalama wa chakula, kusoma na kuandika, na viashiria vingine mbalimbali. Mawasiliano yalifanywa na kanisa katika eneo tofauti la nchi na mchungaji alitumwa kupanda kanisa la kwanza katika eneo hilo. Wafanyakazi Wakristo walimuunga mkono yeye, familia yake, na ushirika huo mpya kwa njia mbalimbali. Upinzani mkubwa ulitokea ndani ya eneo hilo na waumini wa kanisa na, kwa kusikitisha, kanisa liligawanyika ndani ya miaka michache kutokana na mzozo kati ya viongozi wawili; wafanyakazi waliendelea kuunga mkono makanisa yote mawili. Karibu miaka ishirini baadaye, kuna makanisa zaidi ya kumi katika eneo hili lenye zaidi ya wanachama 200. Maboresho makubwa ya maendeleo yameendelea katika eneo hilo kupitia kazi ya serikali na mashirika kadhaa yasiyo ya kiserikali. Makanisa kadhaa pia yanahudumia jamii zao kubwa kwa njia mbalimbali.*

Kama Mark Galpin anavyosema katika shahidi asie gawanyika, hadithi hii inaonyesha changamoto na fursa kati ya maendeleo ya jamii na upangaji wa kanisa miongoni mwa jamii ambazo hazijafikiwa na injili.

Je, ni changamoto gani ambazo mashirika ya umisheni yalikabiliana nazo?

MAJIBU YAKO:

- ✓
- ✓
- ✓

6. Kuna viwango tofauti tofauti vya upya (au mabadiliko) vinavyotokea katika jamii. Kwetu sisi, kama wafuasi wa Yesu, kuna viwango tofauti vya uhuru wa kutangaza, kwa nyakati tofauti.

Ni katika maeneo gani unataka watu katika jamii yako wapate upya, au uhuru?

MAJIBU YAKO:

- ✓
- ✓
- ✓

## Kuwa tayri kila wakati

7. Kanuni ya Saba inaelekeza kwenye hitaji la maono, na kuwa na nia. Hilo linajumuisha kuwa tayari. Hebu tuangalie kile Petro anachosema kuhusu hili.

Badala yake, ni lazima umwabudu Kristo kama Bwana wa maisha yako. Na kama mtu akikuuliza kuhusu tumaini lako kama mwamini, uwe tayari sikuzote kulieleza. Lakini fanyeni hivi kwa upole na heshima. Wekeni dhamiri zenu safi. Ndipo watu wakikutukana, wataaibika watakapoona jinsi unavyoishi maisha mazuri kwa sababu wewe ni wa Kristo.

8. Inamaanisha nini 'kuwa tayari' kuelezea? Inaendanaje na wazo letu la 'kuonyesha na kuelezea' habari njema kwa njia isiyogawanyika?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓

9. Tunatambuaje fursa za kuelezea tumaini tulilonalo? Tunajuaje kama tunapaswa kushiriki au la?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓

10. Je, wakati mwingine umehisi kupata fursa ya 'kuelezea tumaini lililo ndani yako' lakini hukuwa na ujasiri?

Tunawezaje kujenga ujasiri huu ili tuwe tayari wakati unaofaa utakapofika? Ni mambo gani maalum unayoweza kufanya ili 'kujenga zana yako' ili uwe tayari kuelezea?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓

11. Inamaanisha nini 'kufanya hivi kwa upole na heshima' katika muktadha wako?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓

## Kuzingatia wakati

12. Tunataka kutumia vyema kila fursa, kuwa na nia na kuwa tayari. Hata hivyo, pia kuna ukweli kwamba kuna nyakati ambapo kuelezea kunaweza kusababisha madhara zaidi kuliko mema. Ni lini hili linaweza kuwa kweli?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓
✓

13. Unalinganishaje kile unachohisi kama fursa katika wakati huu dhidi ya mawazo ya muda mrefu?

Katika sura hii kuhusu 'uinjilisti wa kimaadili' katika Ushahidi Usiogawanyika, Mark Galpin anarejelea mwitikio tofauti—angalau kwa wakati—kwa hadithi aliyosimulia hapo awali, iliyonukuliwa mwanzoni mwa majadiliano yetu.

*Mara baada ya matetemeko ya ardhi ya Nepal ya 2015, mashirika mengi ya Kikristo yalikuja nchini kutoa msaada. Katika mkutano wa mashirika ya misaada ya Kikristo niliyohudhuria, mwakilishi mmoja wa shirika alishiriki kwamba juhudi zao zilikuwa zikienda vizuri lakini, kama alivyosema, 'waliona ni changamoto kuunganisha uinjilisti na usambazaji wetu wa misaada'.*

*Nikiwa mmoja wa wachache katika chumba hicho wenye uzoefu wa zaidi ya wiki chache huko Nepal, nilijibu kwa nguvu sana, nikiweka wazi kwamba katika hali yoyote hawapaswi kujaribu kuunganisha uinjilisti na msaada wao. Kwa nini nilihisi sana kuhusu hili? Nilijua sana kwamba huko Nepal ni shutuma ya kawaida sana inayoelekezwa kwa mashirika ya Kikristo kwamba 'wanawashawishi' na kuwalazimisha watu kuwa Wakristo. Baada ya tetemeko la ardhi, serikali ilikuwa ikifuatilia hili kwa karibu sana. Dokezo lolote la kushawishi watu wa dini lingeharibu sifa si tu ya shirika lililohusika moja kwa moja bali pia Wakristo wengine wote. Lingeleta athari mbaya kwa mtazamo wa injili yenyewe, na kuna uwezekano mkubwa lingesababisha kupigwa marufuku kwa ushiriki wowote wa wakristo katika juhudi za kutoa misaada na ujenzi upya, na kupunguza msaada na usaidizi uliohitajika sana.*

*Kanisa la mahali hapo huko Nepal lilikuwa limechukua msimamo wazi kwamba huu ulikuwa wakati wa kukidhi mahitaji ya kimwili ya watu, na si kushiriki katika kutangaza. Kwa kufanya hivi, walikuwa na uhakika kwamba, katika hali hii, walikuwa wakishuhudia ipasavyo upendo alio nao Kristo kwa watu wote wa imani yoyote. Wakati wa kutangaza ungefika; huu ulikuwa wakati wa kuonyesha.*

*Shirika lililotajwa halikuwa na uelewa wa muktadha. Mbinu yao iliendeshwa na hitaji la kuhisi kwamba walikuwa wakifanya 'ujumbe kamili' wenyewe katika hali hii. Hii ilitokana na uelewa mdogo wa Ufalme wa Mungu. Kwa hivyo, walileta madhara zaidi kuliko mema.*

A. Kulingana na hadithi hii, ni nini kilikuwa sahihi na ni nini kilikuwa si sahihi na mtazamo wa shirika la nje? Hadi wakati wa mkutano, walikuwa wamemsikiliza nani?

MAJIBU YAKO:

- ✓
- ✓
- ✓
- ✓

B. Mtazamo wa kanisa la Nepal ulikuwaje? Maono yao yalikuwaje? Kwa nini mtazamo wao ulikuwa muhimu?

MAJIBU YAKO:

- ✓
- ✓
- ✓
- ✓

C. Hadithi hii inatuambia nini kuhusu mchanganyiko wa a) nia na maono pamoja na b) mtazamo wa muda mrefu na usikivu wa wakati?

MAJIBU YAKO

- ✓
- ✓
- ✓
- ✓

D. Hadithi hii inashauri nini kuhusu jinsi mtendo na maelezo ya habari njema yanavyoendana?

MAJIBU YAKO

- ✓
- ✓
- ✓
- ✓

## Hitimisho

14. Sehemu ya mwisho ya 1 Petro 3:16 inatuambia 'Tuwe na dhamiri safi. Ndipo watu watakapowatukana, wataaibika watakapoona jinsi mnavyoishi maisha mema kwa sababu ninyi ni wa Kristo.'

    Kwa nini ni muhimu kwetu kuishi maisha mazuri miongoni mwa watu katika jamii yetu? Nini kitatokea tusipofanya hivyo?

15. Ni jambo gani moja linalokuvutia kutokana na mjadala wa leo? Umejifunza nini ambacho unafikiri wewe na timu yako mnaweza kukitumia kwa vitendo?

## Kwa ajili ya kutafakari kibinafsi:

Katika kipengele hiki tumezungumzia umuhimu wa kuwa na maono wazi na kuwa na nia ikiwa tunatamani kuona mabadiliko yakitokea. Je, hii ni kweli kuhusu timu yako na wewe? Unaweza kuboresha kwa njia gani?

Unaonaje jamii za wafuasi wa Yesu
zikichangia mabadiliko katika jamii unayoishi au unayotumikia?

Kwa masomo zaidi...

*Sura ya Saba na Tafakari kuhusu Uinjilisti wa Maadili, Ushahidi Usiogawanyika.*



# Kanuni ya Nane: Wafanyakazi wa maendeleo ya jamii wamejitoa kufanya kazi kwa ubora wa kitaaluma (weledi).

Malengo ya Majadiliano Haya:

1. Timu itakuwa na uelewa mzuri wa jinsi kazi inavyoweza kuwa kielelezo cha ibada.
2. Pia tutakuwa na uelewa mzuri wa maana ya uweledi na kwa nini ni muhimu tunapohudumia jamii zetu.

## Mapitio

1. Wiki iliyopita tuliangalia Kanuni ya Saba: 'Mabadiliko ya kweli yanahitaji maono kwa jamii za wafuasi wa Yesu na upya wa watu binafsi na jumuiya.'

Tafakari ya kibinafsi ilikuwa kuzingatia kama aina hii ya maono na nia ni kweli kwa timu yako na wewe. Unaweza kuboresha kwa njia gani?

Unaonaje jamii za wafuasi wa Yesu zikichangia mabadiliko katika jamii unayoishi au unayotumikia?

Tuchukue dakika 3-4 kushirikisha jinsi tulivyojibu swali hilo.

## Ubora wa Kitaaluma ni nini? (Uweledi).

2. Wiki hii tutaangalia Kanuni ya Nane.

Muhtasari wa Kanuni ya Nane: *'Wafanyakazi wa maendeleo ya jamii wamedhamiria ubora wa kitaaluma (weledi).'*

3. Tuanze kwa kuelewa tunachomaanisha kwa kusema ubora wa kitaaluma. Unawezaje kufafanua neno 'taaluma'?

MAJIBU YAKO:

4. Muhula unaofuata tunachotaka kuuangalia ni neno 'ubora'. Unaelewaje wazo la ubora?

MAJIBU YAKO:

5. Mara nyingi watu hushangazwa na ubora kwa sababu ubora unazidi kiwango cha chini cha kile kinachohitajika.

   A. Hebu tufikirie hadithi katika Biblia ya Ruthu. Mambo yangekuwa tofauti sana kama Ruthu na Boazi wangefanya kwa kiwango cha chini kabisa kilichohitajika na jamii au katika sheria.

   B. Ni kwa njia gani Ruthu alizidi kile kilichotarajiwa?

   C. Vipi kuhusu Boazi? Ni kwa njia gani alifanya zaidi ya kile kilichohitajika?

   D. Nini yalikuwa matokeo ya kufanya kwao zaidi?

6. Tunaweza kusema kwamba matendo ya Ruthu na Boazi yalikuwa matendo ya ibada kwa sababu yalimletea Mungu utukufu. Matendo yao yalionyesha upendo wake mwaminifu wa kujali. Kazi yetu inaweza pia kuwa kitendo cha ibada. Unaonaje kazi unayofanya kama kitendo cha ibada?

MAJIBU YAKO:

- ✓
- ✓
- ✓

7. Kazi ilikuwa zawadi kutoka kwa Mungu, iliyotolewa kwa Adamu na Eva kabla ya Kuanguka. Kazi tunayofanya si tu 'uovu wa lazima' unaotokana na dhambi.
   - Maandiko yanatuambia kwamba chochote tunachofanya, tunapaswa kukifanya kwa moyo wote, kama kufanya kwa Bwana. (Kol. 3:23)
   - Maandiko pia yanatuambia kwamba sisi ni makuhani wa kifalme. (1 Petro 2:9) Hii inarejelea maisha yetu yote, na si shughuli maalum tu zinazofanywa katika mazingira ya kidini.

8. Tufikirie kuhusu kazi tunayofanya. Katika kazi yetu, mara nyingi kuna viwango vinavyowekwa kwa ajili yetu (na serikali, mashirika ya kitaaluma, vyama, mashirika, miungano, watu wanaotoa ithibati, n.k.). Kwa mfano, katika nchi nyingi unahitaji kuendelea na usajili wako kama muuguzi au mtaalamu wa tiba ya viungo. Unaweza kuwa na sifa kamili, lakini bado unahitaji usajili wa ndani.

   Je, ni viwango gani vya kitaaluma vilivyowekwa kwa ajili yetu na watu wanaofanya kazi kama hiyo katika jamii yetu? Huenda hata vikawa viwango vilivyowekwa na timu yako au uongozi.

   MAJIBU YAKO:

   - ✓
   - ✓
   - ✓
   - ✓

9. Kwetu sisi, kama wafuasi wa Yesu, kuna viwango vingine vinavyotegemea maadili ya kibiblia. Kwa mfano, tunaambiwa katika maandiko kuwa wepesi wa kusikia, si wepesi wa kusema na si wepesi wa kukasirika (Yakobo 1:9). Ni viwango gani vingine vinavyoweza kuwekwa kulingana na maadili ya kibiblia?

   MAJIBU YAKO:

   - ✓
   - ✓
   - ✓

10. Tuna wadau wengi.

*Wadau ni watu wenye nia katika mradi au shughuli. Wanaweza kuathiriwa (kwa uzuri au ubaya) na matokeo ya mradi. Wadau ni pamoja na jamii inayohudumiwa, watu wa nje wanaosaidia katika mradi, serikali za mitaa, wafadhili, na wengine. 'Wadau muhimu' ni wale watakaoathiriwa zaidi na mradi au ambao wamefanya uwekezaji mkubwa zaidi ndani yake.*

Jamii tunayoihudumia mara nyingi ndiyo wadau wanaosahaulika. Tunataka kuwathamini. Wameumbwa kwa mfano wa Mungu. Watu wengi huja katika jamii yao na 'kuwaambia' tu wanachohitaji lakini tunatakiwa kuwasikiliza. Mungu tayari amewapa uwezo wa kufanya mema ndani yao na kuyafanya kwa ubora; tunataka kusaidia kuibua ubora ulio ndani yao. Yote haya yanaonyesha hamu yetu na hitaji la kukuza uhusiano nao. Hilo litakapotokea, badala ya kitu kinacholazimishwa kutoka nje ya jamii hiyo (sio watu wa nje) tutakuwa wamiliki na viongozi wa kweli wa kinachotokea.

11. Fikiria kuhusu miradi tunayohusika nayo (au tunayoijua au tunayoweza kushiriki). Wadau ni akina nani?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

Katika hali yetu maalum, wadau wetu muhimu katika jamii wanapaswa kutarajia nini kutoka kwetu tunapohusiana nao?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

12. Gabriel Markus anasimulia hadithi muhimu kuhusu jamii tunayoitumikia kama wadau.

*Kama ilivyotajwa hapo awali katika mafunzo yetu, niliratibu mradi mkubwa wa ujenzi nchini Sri Lanka baada ya tsunami ya Siku ya Ndondi ya 2004 kuwaacha maelfu bila makazi. Asubuhi moja nilipokea simu ya dharura kutoka kwa mfanyakazi katika shirika la washirika wa Ulaya: mtu huyo alikuwa ameishiwa na pumzi, akinisihi nije haraka kwa sababu mtu alikuwa akimfukuza na kutishia kumuua kwa koleo.*

*Niliingia haraka kwenye gari langu, nikaendesha gari hadi eneo la tukio, na niliweza kutuliza mambo. Mtu huyo wa Ulaya hakujua alikuwa amefanya kosa gani, kwa nini mtu huyo alikuwa na hasira sana—lakini alihisi kwamba mtu huyo wa Sri Lanka hakuthamini kazi yao ngumu. Nilimgeukia Msri Lanka na, nikizungumza kwa lugha yake, nikamuuliza kuhusu hili. 'Tunashukuru,' alisema, 'lakini hawasikilizi.'*

*Ilibainika kuwa Wazungu walikuwa na mpango mzuri wa sakafu kwa ajili ya nyumba—lakini walikosea kipengele kimoja muhimu. Kwa wanakijiji wa Kitamil wa Kihindu, ilikuwa ni muhimu sana mlango wa nyumba yao uelekee mashariki ili kupokea baraka ya jua linalochomoza (bila kujali mtaa wa karibu uko wapi). Kushindwa kusikiliza kwa wazungu kulikuwa karibu kusababisha ujenzi wa nyumba ambazo zisingethaminiwa (na pengine kupoteza maisha ya mfanyakazi mmoja wa NGO).*

Hadithi hii inaeleza umuhimu muhimu wa kusikiliza jamii tunazozihudumia na kujua ni nini muhimu kwao. Zaidi ya utaratibu huu muhimu, katika hali yetu mahususi, wadau wetu muhimu katika jamii na pamoja na wengine (kama wafadhili na maafisa wa serikali) wanapaswa kutarajia nini kutoka kwetu tunapohusiana nao?

MAJIBU YAKO:

## Hitimisho

13. Kwa hivyo tunaona kwamba kuna matarajio ambayo yamewekwa kwetu na timu yetu, na mamlaka za nje, kutoka kwa jamii na kutoka kwa wengine akiwemo Mungu mwenyewe.

Fikiria kuhusu jukumu lako mwenyewe. Hili linaweza kuwa kuhusu kazi yoyote unayofanya, si maendeleo ya jamii pekee. Unapoendelea na kazi yako, kuna tofauti gani kati ya kufanya kwa kiwango cha chini cha kile kinachotarajiwa na kutumikia kwa ubora?

MAJIBU YAKO:

14. Kuna tofauti gani katika ushuhuda wetu tunapojitolea kwa ubora wa kitaaluma?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓
✓

15. Ni wazo gani lililokuvutia kutoka kwa mjadala wa leo? Kwa nini?

## Kwa ajili ya kutafakari kibinafsi:

Katika mazingira ambayo ninahudumu, au ninatumaini kuhudumu, je, kuna maeneo ambayo ninahitaji kuboresha mafunzo yangu ya kitaaluma? Ninawezaje kukuza ujuzi huo? Kwa kuwa siwezi kufanya kila kitu mwenyewe, ni katika maeneo gani mimi (au timu yangu) ninahitaji kupokea msaada na ushauri kutoka kwa wale wenye ujuzi wa kitaaluma?

## Kwa masomo zaidi.......

*Sura ya Nane, Ushahidi Usiogawanyika.*



# Kanuni ya Tisa: Kanuni za ubora/uweledi za pamoja

Malengo ya Majadiliano Haya:

1. Watu katika timu wataona jinsi Maendeleo ya Jamii na Kanuni za VCJF zinavyosaidiana.
2. Watu katika timu wataona jinsi Maendeleo ya Jamii yanavyochanganyika katika vitendo na juhudi za kuona jamii za wafuasi wa Yesu zikiundwa na kukua.

## Mapitio (dakika 5)

1. Wiki iliyopita tuliangalia Kanuni ya Nane: Wafanyakazi wa maendeleo ya jamii wamejikita kwenye ubora wa kitaaluma. Tafakari ya kibinafsi ilikuwa kuzingatia maeneo ambayo ninahitaji kuboresha mafunzo yangu ya kitaaluma. Ninawezaje kukuza ujuzi huo? Kwa kuwa siwezi kufanya kila kitu mwenyewe, ni katika maeneo gani mimi (au timu yangu) ninahitaji kupokea msaada na ushauri kutoka kwa wale wenye ujuzi wa kitaaluma?

2. Tuchukue dakika 3-4 kushirikisha jinsi tulivyojibu swali hilo.

## Utangulizi (dakika 3)

3. Wiki hii tutaangalia Kanuni ya Tisa.

Muhtasari wa Kanuni ya Tisa: 'Kuna kanuni nyingi za pamoja za ubora kati ya maendeleo ya jamii na kuunda jumuiya zenye nguvu za wafuasi wa Yesu.'

4. Hebu tusikie uzoefu wa Andrea katika sikuku moja ya Krismasi huko Asia ya Kati na tuone tunachoweza kujifunza kujihusu.

*Mkesha mmoja wa Krismasi katika mji mdogo huko Asia ya Kati, Andrea alipika chakula kutoka nchi yake ambacho alifikiri hakingekuwa cha ajabu sana kwa marafiki zake wa eneo hilo: kuku wa kuchoma, wali wa kuchemsha na mboga.*

*Kama ilivyokuwa desturi ya eneo hilo, alitandaza kitambaa cha meza sakafuni na kwa fahari akawapa marafiki zake wa eneo hilo chakula hicho. Walihamisha chakula hicho kwenye sahani zao kwa bidii; wechache walikula kuku lakini wachache waligusa kilichobaki.*

*Andrea alipoteza uvumilivu na kuuliza, "Kwa nini hamli hiki? Kina viungo sawa na pilau ya kuku!" Akiwa ameshangaa, marafiki zake walimtazama Andrea na kusema, "Ndiyo, lakini ikiwa ulijua hilo, basi kwa nini ulipika kila kitu tofauti wakati ungechanganya kingekuwa kitamu zaidi?"*

A. Hii inakufanya ufikirie nini kuhusu maisha yako mwenyewe? Je, maisha yako ni kama kitoweo, kila kitu kinapikwa pamoja, au ni kama mlo na kila kitu kimepikwa vipande tofauti?

MAJIBU YAKO:

- ✓
- ✓
- ✓
- ✓

B. Kuna faida gani kuwa kama kitoweo? 'Kupikwa' vipande tofauti?

MAJIBU YAKO:

- ✓
- ✓
- ✓
- ✓

5. Unapofikiria kuhusu mijadala yetu, hadithi hii inakufanya ufikirie nini kuhusu 'ushahidi usiogawanyika', 'kuonyesha na kuelezea habari njema', maendeleo ya jamii, na jamii za wafuasi wa Yesu?

MAJIBU YAKO:

- ✓
- ✓
- ✓
- ✓

## Kanuni za Kulinganisha

6. OM imeunda orodha ya ‘kanuni kumi za VCJF za kusaidia kuunda huduma yetu’. Kanuni hizi zina mwingiliano mwingi na kanuni bora za maendeleo ya jamii.



| | |
|---|---|
| Kanuni ya Kanuni ya VCJF | Kanuni inayotumika kwa mabadiliko na maendeleo ya jamii. |
| Maombi na kufunga | Tunawatunza wajane na yatima, iliyoelezwa kama funga ya kweli katika Isaya, na tunaposhiriki katika mabadiliko ya maendeleo, tunahitaji kufahamu mtazamo wa ulimwengu wa kiroho na nguvu katika jamii. (Tazama Sura ya 5) |
| Ushirikiano | Tunashirikiana na jamii na wadau wote. Maendeleo yanapaswa kuwa mchakato unaojumuisha kila wakati. |
| Jiandae kuteseka | Tunaishi miongoni mwa wale wanaoteseka na kuomboleza pamoja na maombolezo, hata kama hii inatuletea hatari. Tunatafuta mtazamo wa kitheolojia kuhusu mateso pamoja. |
| Fanya kile kinachoweza kuzalishwa kwa urahisi. | Miradi yetu ya maendeleo inategemea mali za ndani na teknolojia inayofaa ambayo inaweza kuzalishwa na kupanuliwa. |
| Kupanda kwetu kwa upana ni muhimu, kwa muktadha na kunatafuta kutoa hatua inayofuata. | Tunaweka uhusiano na muktadha wa muhimu katika ukweli wa kiroho katika mtandao mpana ulijengwa kupitia ushirika wetu na jamii. |
| Tunaingia na tunashirikiana na jamii ambazo hazijafikiwa. | Jamii ambazo hazifikiwi mara nyingi sana ndio jamii ambazo hazijafikiwa katika maendeleo, elimu na uchumi. Hasa katika maeneo maskini zaidi duniani, kuishi katika jamii kama mfanyakazi wa maendeleo kunatupa uwepo halisi. |
| Unda na utumie timu ipasavyo. | Maendeleo ya jamii ni kazi ya pamoja na tayari mara nyingi ni kazi ya pamoja ya tamaduni nyingi na mashirika mbalimbali. |
| Zingatia vikundi. | Tunatekeleza uundaji wa jamii na kuiga jamii zenye afya za usaidizi wa rika na ujifunzaji wa rika katika miradi yetu. |
| Fanya wanafunzi, si waongofu. | Maendeleo ya jamii huwaona washiriki kama wakala wa mabadiliko, watu wenye uwezo wa kubadilisha na kubadilisha jamii zao mbalimbali. |
| Uongozi wa ndani na umiliki. | Maendeleo ya jamii ni msaada wa muda. Tunaiga, tunasaidia, tunaongoza na kuunda mwanzo wa viongozi wa jamii wenye mwendelezo. Kama mashirika ya maendeleo ya Kikristo, tunaiga na kufundisha uongozi wa watumishi na wachungaji kwa ngazi zote za jamii. |

7. Unapoangalia orodha hii, kwa namna gani kulinganisha seti mbili za kanuni kunaonyeshaje kwamba ‘hatujagawanyika’ katika ushuhuda wetu?

MAJIBU YAKO:

- ✓
- ✓
- ✓

8. Hebu tuangalie baadhi ya kanuni hizi kwa undani zaidi. Mwandishi wa Sura ya 9 katika kitabu cha Mashahidi wasiogawanyika aliandika yafuatayo, akimtumia mtaalamu wa maendeleo ya mabadiliko Bryant Myers:

Mojawapo ya kanuni muhimu zaidi katika maendeleo ya jamii ni ushiriki hai wa jamii katika kutafuta suluhisho na kuweka ajenda na mwelekeo wa mchakato wowote wa maendeleo. Bryant Myers anatukumbusha katika kitabu chake Walking with the Poor (kuembea na masikini) (ukurasa wa 218) kwamba ikiwa tunataka kushiriki hadithi zetu kwanza tunahitaji kusikiliza hadithi zao. Kisha Bryant Myers anasema:

> *'…tunakabiliwa na changamoto. Tunawezaje kuunganisha hadithi hizi ili ziweze kukuzana, na kila mtu anajifunza na kukua? Jambo la msingi ni kuwa jamii kwa kila mmoja…Kujenga jamii ni kile majirani wema hufanya.'*

A. Unaona wapi ushiriki hai wa jamii unaofaa katika maendeleo yako ya jamii au kazi kama hiyo? Tunasikilizaje hadithi yao na kuwa jamii?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

B. Kwanamna gani au wapi unaliona hili katika uundaji wa makanisa mapya au jumuiya za wafuasi wa Yesu?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

9. Kanuni nyingine muhimu katika maendeleo ya jamii ni uzalishaji na uenezaji. Je, uingiliaji kati yako utachukuliwa na jamii ya wenyeji na kuzalishwa tena ndani ya jamii husika? Je, ni rahisi vya kutosha, kwa kutumia rasilimali zinazopatikana ndani ya nchi? Je, mtu anaweza kuzalisha unachokionyesha?

- Hii inatumikaje kwa aina ya kazi unayofanya?
- Vipi kuhusu mbinu yako katika kuwasaidia watu kukua katika imani, ufuasi?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

10. Mmoja wa wafanyakazi wenzetu wa OM ni mtaalamu wa tiba ya viungo aliye na leseni na utaalamu katika kuwasaidia wale wenye ulemavu. Aliandika:

*Msingi wa maendeleo ya jamii ni wazo kwamba vikundi vya afya, ukarabati, elimu, na vya kujisaidia viko moja kwa moja karibu na watu wanaohitaji huduma hizo. Katika hili, tunazungumzia afya ya msingi dhidi ya kliniki kubwa katika jiji la karibu, shule za vijijini zilizoanzishwa hata katika mazingira ya mbali au ya kuhamahama, elimu jumuishi kwa watoto wenye ulemavu badala ya malazi na chaguzi za elimu maalum, na upatikanaji wa usaidizi wa kisheria na rika kupitia vikundi vya kujisaidia vya wanawake wa eneo husika badala ya kutengwa.*

A. Hii inatumikaje katika mazingira yako kwa huduma na njia unazotaka kusaidia jamii kupata suluhisho kwa mahitaji yao?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

C. Inatumikaje katika kuunda jamii za wafuasi wa Yesu?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

11. Baada ya kujadili thamani ya "kupanda mbegu" kwa upana kupitia vyombo vya habari n.k., mtaalamu wa tiba ya mwili pia aliandika:

*Kazi ya maendeleo ya kidunia mara nyingi huzingatia suluhisho za vitendo, kiufundi na maarifa. Hata hivyo, katika tamaduni nyingi swali la msingi kuhusiana na hitaji la maendeleo mara nyingi huwa la kimahusiano na kiroho. Kama Wakristo, tunaweza kujibu maswali hayo ya kiroho ya msingi ya 'Nani aliyetenda dhambi: mtu huyu au wazazi wake?' (Yohana 9:2). Kushirikisha habari njema zinazohusiana na maendeleo na mtazamo wa ulimwengu katika vikundi na mitandao ya kijamii husaidia kutambua wale wanaomtafuta Mungu na ukweli kwa bidii. Kwa kupanda mbegu zinazofaa katika mtandao mpana wa wanawake, wakulima, na wazazi pamoja na kuendelea kumwagilia mbegu hizi kupitia ushirika na vikundi, wale walio tayari kwa hatua inayofuata ya kusoma neno la Mungu mara kwa mara hujitokeza. Kuingiliana na neno la Mungu huleta mabadiliko ya mtazamo wa ulimwengu na, kwa baadhi, mabadiliko ya utii na utawala. mabadiliko haya husababisha mabadiliko ya tabia na mabadiliko ya kudumu katika jamii nzima kama matokeo ya utii kwa neno la Mungu.*

A. Hii inakuhusuje? Kwa namna gani hii inafanyakazi kwako? Je, 'unapanda' mawazo na taarifa muhimu zinazochangia mahitaji kutimizwa na mabadiliko katika jamii?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

B. Je, kupanda mbegu kwa njia inayofaa katika mtandao mpana kunasababisha baadhi kuwa wafuasi wa Yesu na jamii za wafuasi wa Yesu kuundwa?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

12. Akiandika kutoka Asia ya Kati na muktadha wa mashirika yasiyo ya kiserikali ya kimataifa yanayolenga maendeleo ya jamii anasema:

*Kwa nini wale wanaohusika na juhudi za maendeleo ya kimataifa tayari wanaiga baadhi ya maadili ambayo kanisa na wale wanaohusika katika utume miongoni mwa wale ambao hawajafikiwi kabisa na injili wanapaswa kuamini kwa undani na kuyakubali kwa urahisi? Hizi ni pamoja na kuwa tofauti na kimataifa, kuwapa nafasi waumini wa ndani kukua, na, wanapata uzoefu, nafasi na fursa ya kutumikia kimataifa. Ikiwa mashirika ya utume na makanisa yanaweza kuwa tofauti zaidi na kuwawezesha—kuwaona wale tunaowafunza kama wafanyakazi wenza katika mavuno na kama viongozi wa baadaye wa jamii na mashirika—tutakuwa tumepiga hatua kubwa.*

A. Je, hii inatumika kwa aina ya kazi yako? Je, unaweza kuzungumza kwa tahadhari na kikundi kuhusu hali ambapo watu wanawezeshwa kukua na kufikia majukumu na uwajibikaji? Ikiwezekana (na kuwafikiria wale wanaohusika) je, kuna hali ambapo hili halifanyiki?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

B. Je, tunashikilia mamlaka, au kuwawezesha wengine kukuza ujuzi wao na kukua katika uongozi? Ni maoni au mifano gani chanya unayoweza kutoa kuhusu jinsi ulivyosaidiwa?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

13. Azimio la Mika linasema:

*Tukipuuza ulimwengu tunasaliti neno la Mungu, ambalo linatutuma kutumikia ulimwengu. Tukipuuza neno la Mungu hatuna cha kuleta duniani. Haki na kuhesabiwa haki kwa imani, ibada na hatua za kisiasa, kiroho na kimwili, mabadiliko ya kibinafsi na mabadiliko ya kimuundo yanaungamanika. Kama ilivyo katika maisha ya Yesu, kuwa, kutenda na kusema ndio kiini cha kazi yetu muhimu.*

- Tunapofikiria kanuni mbalimbali za maendeleo mazuri ya jamii zilizoorodheshwa hapo juu, je, unaziona zikiendana vizuri na jinsi tunavyoshuhudia?
- Je, mifano hii mizuri ya matendo na maelezo ya habari njema yanaendana vizuri?
- Unaona wapi mwingiliano katika kile unachokifanya kama wafanyakazi bora wa maendeleo ya jamii (au jukumu linalofanana) na kile unachofanya (au unachopaswa kufanya) katika suala la kuona jamii mpya, zenye wafuasi wa Yesu zikiundwa?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓

## Kutekeleza (dakika 10)

14. Tufanye hili liwe la vitendo kwa kufikiria jinsi tunavyoweza kutumia mawazo haya.

- Tunaweza kufanya nini tofauti?
- Tutatekelezaje mabadiliko?
- Ni nani katika timu yetu atakayewajibika kwa sehemu gani?
- Mabadiliko haya yataanza kutumika lini?

MAJIBU YAKO:

- ✓
- ✓
- ✓

## Hitimisho (dakika 10)

15. Tumalizie kwa kusoma hadithi hii, uzoefu wa mmoja wa mfanyakazi mwenzetu.

*Miezi michache iliyopita nilitembelea familia ya wakimbizi katika jiji la Mashariki ya Kati, pamoja na timu ya shirika letu lililojumuisha daktari wa watoto wa Magharibi na mfamasia wa Mashariki ya Kati. Wote wawili walizungumza Kiarabu na Kiingereza vizuri na waliwapenda sana watu waliokuwa wakiwahudumia. Tulitembelea familia inayoishi katika umaskini mkubwa: mwanamke huyo alikuwa akikabiliwa na matatizo katika ndoa yake na Watoto wake wanne kati ya sita walikuwa na ulemavu au sifa za unyanyapaa kama vile ualbino. Ingawa niliona, timu hiyo ilisikiliza na kumfariji, walitoa ushauri bora wa kimatibabu na rufaa, na ikamsaidia mwanamke huyo asiyejua kusoma na kuandika kusoma karatasi za kimatibabu. Walishiriki tabasamu pamoja na wawili hao waliimba nyimbo chache na watoto na kutoa mazoezi kwa msichana aliyeonekana kuwa na ugonjwa wa kupooza ubongo. Mwishoni mwa ziara yetu, jirani alikuja. Mfanyakazi mwenzangu yule Mwarabu alisimulia hadithi ya Yesu, akajibu maswali zaidi, na akaomba baraka kwa familia hiyo. Kisha tukaondoka.*

*Ni mara chache nimeona yote niliyoandika hapo juu yakiishi katika nafasi na wakati mdogo kama huo—misheni muhimu ikiishi na kuonekana katika ziara ya dakika sitini, karamu ya ladha na ladha iliyochanganywa vizuri na kumpendeza mwanadamu na Mungu.*

*Tuweke pamoja kile kinachostahili kuwa pamoja; mambo huwa matamu zaidi yakichanganywa vizuri!*

## Kwa ajili ya kutafakari kibinafsi:

Wiki hii tumezingatia kufanana kwa kanuni za maendeleo bora ya jamii na kwa ajili ya uundaji wa jamii za wafuasi wa Yesu.

Je, kuna kanuni yoyote kati ya hizi iliyokuvutia? Ni zipi? Kwa nini?

Je, unafikiri kwamba Mungu anataka uyatekeleze au ufanye mabadiliko? Ikiwa ndio, andika mawazo machache kuhusu unachohisi. Unaweza kushirikisha mawazo haya na nani kisha uombe pamoja naye ili njia ya Mungu isonge mbele?

## Kwa masomo zaidi...

Sura ya Tisa, Shahidi Asiyegawanyika.



# Kanuni ya Kumi: Wale wasiofikiwa wapo kwasababu.

Malengo ya Majadiliano Haya:

1. Timu yetu itaweka mawazo yetu wazi tunapofikiria wasiofikiwa ni kina nani?.
2. Watu katika timu yangu watakuwa na uelewa mzuri wa kwa nini watu hawajafikiwa.
3. Timu yetu itakuwa na ufahamu mpya wa vikwazo vya kufikia wale wasiofikiwa hata kidogo.
4. Watu katika timu yangu watakuwa na uelewa mzuri wa jinsi sisi wenyewe tunayo mengi ya kujifunza kutoka kwa wale wasiofikiwa hata kidogo, jinsi Mungu anavyoweza kuwatumia kutubadilisha.

## Mapitio

1. Wiki iliyopita tuliangalia Kanuni ya Tisa. Tafakari ya kibinafsi ilikuwa kuzingatia ni kanuni zipi zilizokuvutia, kanuni za ubora katika maendeleo ya jamii zinazoingiliana na kanuni za uundaji wa jumuiya zenye nguvu za wafuasi wa Yesu.

   Ni kanuni gani/kanuni zipi zilizokuvutia? Kwa nini?

   Unadhani ni mabadiliko ya aina gani ambayo Mungu angependa uyatekeleze?

2. Tuchukue dakika 3-4 kushirikisha jinsi tulivyojibu maswali haya.

## Utangulizi

3. Wiki hii tutaangalia Kanuni ya Kumi.

Muhtasari wa Kanuni ya Kumi: ‘Wale wasiofikiwa hata kidogo wapo kwa sababu fulani.’

## Sehemu ya Kwanza: Wasiofikiwa hata kidogo ni kina nani? (Dakika 10)

4. Kifungu cha maneno ‘wasiofikiwa hata kidogo’ kinakudokezea nini?

MAJIBU YAKO:

✓

✓

✓

5. Katika OM, tulifafanua ‘wasiofikiwa hata kidogo’ kwa upande wa jamii ambapo

- Hakuna mtu anayeshirikisha kuhusu Yesu.
- Hakuna jamii ya wafuasi wa Yesu inayoshirikisha mafundisho yake.
- Vizuizi kama vile lugha na utamaduni hutenganisha watu na wafuasi wa Yesu wa eneo hilo.

6. Mara nyingi, tunapotumia maneno kama 'wasiofikiwa' na 'wasioinjilishwa' tunatumia namba kubwa, 'asilimia ya idadi ya watu wa kiinjilisti' na takwimu zinginezo.

Lakini katika OM, tulipofafanua 'wasiofikiwa sana' tulitaka kuizungumzia kama wazo kwamba hilo linahitaji kulinganishwa: 'jamii hii haijafikiwa hata kidogo kuliko jamii hiyo'. Hatukutaka neno hilo lifafanuliwe kwa takwimu na nambari zilizohesabiwa na kundi fulani la nje, au kuwekwa bandia kulingana na makundi ya kikabila au makabila.

A. Mtazamo wa 'idadi kubwa' wa kitakwimu una athari gani katika njia yetu ya kufikiria kuhusu wale wasiofikiwa hata kidogo?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓

B. Ni kwanamna gani Mungu anataka tufikirie kuhusu ambao hawajafikiwa?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓

7. Kwa kuzingatia hilo,

- Wasiofikiwa hat akidogo ni kin nani?
- Je, wanaukaribu nawe, au wako mbali?
- Ikiwa tunaweza kuwafikiria watu kama 'Waarabu huko Afrika Kaskazini' au 'Wabudha huko Tibet' kama wasiofikiwa hata kidogo, kina nani wanaweza kuwa hawajafikiwa hata kidogo walioko karibu nawewe, labda wamefichwa kutoka kwa mtazamo wa wakristo katika eneo lako?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

## Sehemu ya Pili: "kwa sababu" (dakika 15)

8. Ni vikwazo gani vinavyosababisha jamii kuto kufikiwa kabisa? Ni nini kinachofanya baadhi ya watu hawa kuwa vigumu zaidi kufikiwa?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

9. Rosemary Hack alisimulia hadithi ya mtu aliyemwita Sally.

*Nitakumbuka kila wakati nilipokutana na Sally kwa mara ya kwanza. Sally ni Muislamu wa Kimalesia; katika nchi yake kuna adhabu kali kwa wote wawili anaeshuhudia na anaeshuhudiwa kwa Kristo. Hata hivyo, Sally ana vikwazo vingine zaidi vinavyomtenganisha na jamii: yeye ni mwathirika na anaishi na VVU..*
*Kukimbia na kujificha kutoka kwa mamlaka, ni vigumu kwake kupata huduma za matibabu, au kuomba ulinzi wa polisi; lazima aepuke polisi kwa kuwa kuambukiwa VVU ni kinyume cha sheria, na watu walioambukizwa mara nyingi hupigwa vikali na wale wanaopaswa kuwalinda. Ni nani atakayempelekea Sally habari njema ya Kristo, kusimama naye na kumtetea haki zake za msingi kama mwanadamu aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu?*

'Baada ya kusimulia hadithi hii, alisema: 'Kuingia katika 'ulimwengu wa Sally' huenda kukatufanya wengi wetu tusiwe na raha sana.'

Unakubali?
Kwa namna gani wale ambao hawajafikiwa hata kidogo hutufanya tusiwe na raha? Na kwanini?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

10. Kwa hivyo, tunapofikiria wasiofikiwa kabisa na vikwazo vinavyovitutenganisha au kuficha, ni vikwazo vya nani? Je, inawezekana kwamba baadhi ya vikwazo hivi ni vikwazo vyangu mwenyewe?

    Ni baadhi gani ya vikwazo ambavyo ni vyangu hasa, na si vyao?

    MAJIBU YAKO:
    ✓
    ✓
    ✓

11. Unafikiri Yesu angekuwa wapi leo? Kwa nini?

    MAJIBU YAKO:
    ✓
    ✓
    ✓

## Sehemu ya Tatu – Ili iweje?

12. Wakati mwingine tunapata wazo kwamba tuna majibu yote, kwamba hatuna cha kujifunza—angalau si kutoka kwa 'jamii isiyofikiwa' tunayotaka kuitumikia. Mwenzangu kutoka Afrika Kusini aliona mtazamo huu kuwa mgumu alipotembelea kambi ya wakimbizi.

    *Kila wakati nilipoendesha gari hadi kambi ya wakimbizi, huwanamuona bibi kizee ameketi kando ya barabara kuu. Hili liliendelea kwa wiki kadhaa hadi niliposikiliza msukumo wa Roho aliyesema: 'Unamwona? Ninamwona. Simama kwaajili yake.'*

    *Siku moja nilimwona, na ilikuwa uzoefu wa kubadilisha dhana. Nilimwona kama Yesu kwangu—mnyenyekevu sana,tukishiriki ubinadamu wetu na kumheshimu kwa jinsi alivyokuwa. Sikumshirikisha injili kwa maneno, lakini naamini hakika nilimwonyesha injili. Kwakweli nilimwona Yesu ndani yake, mdogo zaidi kati ya hawa. Labda wasiofikiwa hata kidogo ndio waliofikiwa zaidi kuliko tunavyofikiria, na tunahitaji kuguswa kwa njia mpya na Yesu ndani yao.*

    A. Mwanamke huyu alijifunza nini kutoka kwa bibi kizee? Sentensi yake ya mwisho inamaanisha nini, kwamba tunaguswa na Yesu kupitia wao?

    MAJIBU YAKO:
    ✓
    ✓
    ✓

B. Umewahi kupitia jambo kama hili? Je, unahitaji kupitia jambo kama hili?

MAJIBU YAKO:

13. Rose anasimulia hadithi ya mabadiliko, hadithi ya mbinu ya kuanzia chini kwenda juu ya watu wanaohitaji kuwasaidia wengine wanaohitaji.

*Katika milima ya Nepal, watu wanaoishi na VVU wananyanyapaliwa sana na wanakabiliwa na ubaguzi. Ingawa nchi inapitia ukuaji wa kanisa wenye nguvu katika maeneo kadhaa, watu wanaoishi na VVU wanaachwa nyuma, wanatengwa na wananyanyapaliwa hata na kanisa—na wao wenyewe, wakiamini kwamba mateso yao yanaonyesha jinsi Mungu anavyojisikia kuhusu wao.*

*Hapo awali, huduma nyingi za VVU zilipatikana tu Kathmandu. Watu wanaoishi na VVU walikuja mjini kwa matibabu au walikufa katika vijiji vyao. Wengi waliishia katika jiji hili kubwa lenye watu wengi bila mtu wa kuwasaidia kupitia mfumo wa hospitali na hakuna malazi ikiwa walikuwa wagonjwa wa nje.*

*Wafuasi wachache wa Yesu, wengi wao wakiwa Wanepali wanaoishi na VVU, walijitolea muda wao na kuwafariji, wakitoa mahali pa kukaa na kuwasaidia wagonjwa wapya hospitalini. Walianza vituo vya nje katika jamii za vijijini kwa saa mengi ya safari zisizofurahshai na hatari.*

*Kujidhihirisha kwa Kristo na kusaidia jamii hii ya Wanepali kulienda sambamba. Wale wanaoishi na VVU wanaowasiliana na huduma wanajua kwamba wanapendwa, kwamba kuna mtu anayewaelewa na atawasaidia licha ya aibu yao na kutengwa na jamii. Katika mikutano ya kila mwezi ya vikundi vya usaidizi, Hahindu, Waislamu, na Wakristo hula, huomba, na kumwabudu Mungu pamoja. Mikusanyiko hii ya watu kutoka imani tofauti na makundi ya watu si ya kawaida; ukweli kwamba wanashirikisha waziwazi mapambano yao na kuomba maombi huongeza upekee wa hali hiyo.*

*Wana mambo mawili yanayofanana: VVU na huduma ya wale wanaowasaidia. Wengi bado hawajaamini lakini wako safarini kumpokea Kristo. Mama mzee wa mteja mmoja hivi karibuni alibatizwa na kuanza kumfuata Yesu. Mwanawe wa kiume aliulizwa kama alikuwa mwamini; jibu lake, 'Bado!' lilikuja na tabasamu na maana kwamba ni suala la muda tu.*

Hebu tufikirie hadithi hii ya jamii isiyofikiwa sana ikifikiwa, kwa kiasi fulani, na habari njema.

A. Tatizo lilikuwa nini, na lilitatuliwaje? Nani alichukua hatua za kubadilisha mambo? ilikuwa rahisi kwao?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓

B. Ni nini kilichowaunganisha watu wa asili ya Kihindu, Kiislamu, na hata Kikristo?

MAJIBU YAKO:

✓
✓
✓

## Sehemu ya Nne - Hitimisho (dakika 10)

14. Rose anahitimisha sura yake kwa kuandika:

*Wale ambao hawajafikiwa sana mara nyingi hufichwa, hutenganishwa si nasi tu bali pia na jamii yao wenyewe na mazingira ya uadui, hatari, magonjwa, jinsia, unyanyapaa, umaskini, na mitego tata ya dhambi. Wakati mwingine hufichwa na upofu wetu wenyewe, au kushindwa kwetu kutazama kwa mtazamo unaowezeshwa na Roho. Tunapofanya juhudi za ziada za makusudi za kuwapata, kuwafuata, kuwaelewa, na kuwatumikia tunaweza kujikuta katika maeneo ambayo hatutarajiwi, kwa maneno ya Bryant Myers [katika mazungumzo na David Greenlee], 'mshangao mzuri' ambao unaweza kufungua mioyo na akili kwa huduma na upendo ambao Kristo anatuamuru kutoa.*

Umewahi kupata aina ya mshangao mzuri ambao Bryant Myers anataja? Tafadhali waambie kikundi kuhusu uzoefu huo.

15. Leo tumeangalia ni NANI ‘wasiofikiwa’ na KWA NINI wawe ‘wasiofikiwa’

Hili linahusianaje na yale tuliyoyazungumzia katika majadiliano yaliyopita?

MAJIBU YAKO:

✓

✓

✓

16. Mazungumzo ya leo yanaleta tofauti gani? Je, kuna kitu tunachotaka kufanya tofauti? Ikiwa ndivyo, nini?

## Kwa ajili ya kutafakari kibinafsi:

Injili ilifika lini katika jamii yako, watu wako, au kijiji chako, au kabila lako? Hilo linaweza kuwa limepita muda mrefu ikiwa unatoka mahali kama Ugiriki; au miaka 200 iliyopita kwa baadhi barani Afrika; au hivi karibuni sana kwa wengine.

Injili ilifikaje katika jamii yako au watu wako? Ilifikaje kwako? Yaani, jamii yako iliachaje 'kuwa haijafikiwa'?

Kwa namna gani hadithi yako mwenyewe, hadithi ya jamii yako, inakutia moyo vipi unapofikiria kuzisaidia jamii zingine kuwa wafuasi wa Yesu badala ya 'kuwa jamii zisizofikiwa?

## Kwa masomo zaidi...

Sura ya Kumi, Shahidi Asiyegawanyika.



# Kuangalia nyuma na yale tuliyojifunza.

Malengo ya Majadiliano Haya:

1. Tutapitia pamoja Kanuni ambazo tumejadili na kuelekeza mambo muhimu ya yale tuliyojifunza.
2. Tutatambua hatua maalum tunazoweza kuchukua ili kuweka yale tuliyojifunza katika vitendo.
3. Tutashirikisha mawazo ya jinsi mafunzo yanavyoweza kuboreshwa kwa wengine watakaoyachukua katika siku zijazo.

## Mapitio

1. Wiki iliyopita tuliangalia Kanuni ya Kumi: 'Wale wasiofikiwa hata kidogo wapo kwa sababu fulani.

   Tafakari ya kibinafsi ilikuwa kujibu: Injili ilifika lini kwa jamii yako, watu wako, au kijiji, au kabila lako? Injili ilifikaje kwa jamii yako au watu wako? Ilikufikiaje? Yaani, jamii yako iliachaje 'kuwahaijafikiwa na injili'?

   Kwa namna gani hadithi yako mwenyewe, hadithi ya jamii yako, inakutia moyo vipi unapofikiria kuzisaidia jamii zingine kuwa wafuasi wa Yesu badala ya 'kutokufikiwa hata kidogo'?

2. Tuchukue dakika 3-4 kushirikisha jinsi tulivyojibu swali hilo.

## Kuangalia Nyuma kwenye Kanuni

3. Tumezingatia Kanuni Kumi za Ushahidi Usiogawanyika, kanuni zinazohusiana na wafuasi wa Yesu na maendeleo ya jamii miongoni mwa wasiofikiwa.

   kuna kanuni yoyote kati ya hizi iliyoonekana kuwa muhimu sana kwako?

   Je, tunaweza kutenganisha kanuni hizo—au zinahitaji kuwekwa pamoja? Nini kitatokea tukijaribu kuzitenganisha?

- Muhtasari wa Kanuni ya Kwanza: ‘Kuelewa ufalme wa Mungu ni msingi’
- Muhtasari wa Kanuni ya Pili: ‘Kuelewa jinsi watu wanavyoingia katika ufalme wa Mungu hujenga jinsi tunavyofanya huduma.’
- Muhtasari wa Kanuni ya Tatu: ‘Injili huathiri mtu mzima kama alivyo na muktadha mzima wa watu.’
- Muhtasari wa Kanuni ya Nne: ‘Tunashirikisha maono mapana ya kumtukuza Kristo watu wanapokuja kwenye imani na jamii zinaathiriwa na ufalme.’
- Muhtasari wa Kanuni ya Tano: ‘Maombi na vita vya kiroho ni sehemu muhimu za mchakato wa mabadiliko’
- Muhtasari wa Kanuni ya Sita: ‘Kutunza uumbaji ni udhiirisho wa ibada, ushuhuda na utii.’
- Muhtasari wa Kanuni ya Saba: ‘Mabadiliko ya kweli yanahitaji maono kwa jamii za wafuasi wa Yesu na upya wa watu binafsi na jamii.’
- Muhtasari wa Kanuni ya Nane: ‘Wafanyakazi wa maendeleo ya jamii wamejitolea kwa ubora wa kitaaluma.’
- Muhtasari wa Kanuni ya Tisa: ‘Kuna kanuni nyingi za pamoja za ubora kati ya maendeleo ya jamii na kuunda jamii zenye nguvu za wafuasi wa Yesu.’
- Muhtasari wa Kanuni ya Kumi: ‘Wale ambao hawajafikiwa wapo kwa sababu.’

## Watu Wote, Mashahidi Wasiogawanyika (dakika 15)

4. Katika Epilogue yake ya kitabu cha shahidi asiegawanyika, Dkt. Paul Bendor-Samuel anasimulia hadithi kutokana na uzoefu wake huko Afrika ya kaskazini, uzoefu ulioipa kitabu hicho kichwa cha.

   *Wale walioalikwa na Mungu kushiriki katika huduma isiyogawanyika pembezoni mwa ushuhuda wa injili imepata mahali pa kujifunza kwa kina na kukua kwa kibinafsi: safari ya ufuasi. Hakika hilo ndilo nililopitia mimi na mke wangu wakati wa miaka kumi na miwili tuliyotumia kufanya kazi Afrika Kaskazini katika muunganisho kati ya maendeleo ya jamii na ukuaji wa jamii za wafuasi wa Yesu. Hadithi inakuja akilini kutoka siku hizo:*

   *Niliitwa kusafiri kutoka mji mkuu hadi mkoa wa mbali ambapo mmoja wa timu yetu alikuwa akifanya kazi huko kwa takriban miaka mitano. Katika miaka miwili iliyopita, kikundi kidogo cha wafuasi wa Yesu kilikuwa kimekua kutokana na ushuhuda wa mtu mmoja ambaye maisha yake yalikuwa yamebadilika. Akiwa ameshikwa mikono yake katika kitengo cha fedha alikokuwa akifanya kazi, alishangaa wakati bosi wake, mmoja wa timu yetu, alipomsamehe na kumpa fursa ya kubadilika. Jibu lake lilikuwa kuomba nakala ya 'kitabu chetu'. Huyo Yesu ni nani ambaye angeweza kumfanya mtu atendewe tofauti na yale ambayo wakubwa wengi wangefanya? Ilikuwa mwanzo wa mchakato wa mabadiliko, kukutana na Kristo ndiko kulikombadilisha yeye, mkewe, na familia yake, na kisha kuanza kuwafikia wengine katika jamii. Baada ya miezi kadhaa, polisi waliamua kwamba imetosha na kundi likafungwa.*

   *Huu haukuwa mwisho wa jambo. Mkurugenzi wa Afya wa Mkoa, rafiki yangu wa karibu nchini, alishtushwa, akakasirika. 'Ulitoa vishawishi gani kumshawishi abadilishe*

*dini yake? Umeharibu utamaduni.' Haraka sana Wizara ya Afya ilijiondoa kutoka kwa miradi yetu yote, na kuacha mustakabali wa shirika hilo ukiwa umekwama. Kwa hivyo nilijikuta nikiendesha gari kwenda kwenye mkutano na gavana wa mkoa, bila kujua ninaendakusema nini. Niliingia katika ofisi yake kubwa na kupokelewa kwa neema. 'Mheshimiwa', nilianza, 'unajua kwamba sisi ni Wakristo, tunaoungwa mkono na makanisa. Daima tumekuwa tukitoa bora yetu kitaaluma, tukitafuta kutumikia kwa uadilifu.*

*Motisha unayoendesha ubora wa kazi yetu ya kitaaluma inatokana na uzoefu wetu wa upendo wa Mungu. Motisha huo una maana kwamba mtu anapotuuliza kuhusu imani yetu, tunapaswa kushirikisha kuhusu upendo ambao tumepokea kwa uhuru. Tunaheshimu kwamba hii ni nchi yako na mna haki ya kutuambia tukae au tuondoke. Hata hivyo, sisi ni watu wakamilifu na hamwezi kutugawanya vipande viwili. Hauwezi kuwa na ubora wa kitaaluma bila nia ya kushirikisha kile kinachotufanya tuwe hivyo.' Kwa neema kubwa, Mheshimiwa alinishika mkono na kutuomba tukae.*

Dkt. Bendor-Samuel kisha akasema kwamba sisi ni 'watu wakamilifu, au la' kabisa' kwa sababu tunaleta injili tukufu.

Tukifikiria majadiliano yetu kupitia programu hii ya mafunzo, inamaanisha nini kuwa 'watu wakamilifu'? Shahidi Asiyegawanyika anamaana gani kwako?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

Hii inahusianaje na mawazo ya vitendo na maelezo ya Injili?

MAJIBU YAKO:
✓
✓
✓

## Kuifanya Kuwa ya Kibinafsi

5. Tafadhali fikiria maswali haya kwa ajili ya kujifunza kwako mwenyewe na uyashirikishe katika kikundi lako na viongozi wa programu hii ya mafunzo.

- Utafiti umekuletea tofauti gani?
- Ni ukweli na taarifa gani umejifunza?
- Una maswali gani yasiyojibiwa?
- Je, kuna ujuzi unaofikiri unapaswa kuuendeleza?
- Unafikiri Mungu anataka ufanye matumizi gani? Timu yako?
- Utafanyaje kuhusu kufayafanyia kazi mambo hayo?

## Asante kwa kushiriki!

Asante sana kwa kushiriki katika programu hii ya mafunzo. Tumetumia nguvu nyingi katika kutengeneza somo hili—na tunakushukuru kwa kuwa umetumia nguvu nyingi katika somo hili!

Tungefurahi sana kusikia kutoka kwako kuhusu jinsi kozi hii imeleta mabadiliko kwako, na jinsi unavyoitumia katika vitendo. Pia tunakaribisha mapendekezo yako ya kuboresha mafunzo haya.

Mwishowe, tafadhali fikiria kusoma kitabu cha Shahidi Asiyegawanyika, kilichochapishwa na Regnum mwaka wa 2020 na kuhaririwa na David Greenlee, Mark Galpin, na Paul Bendor-Samuel. Kinapatikana kupitia wachapishaji wa Regnum nchini Uingereza na kupitia maduka mbalimbali ya vitabu mtandaoni kama kitabu cha kuchapishwa na katika umbizo la vitabu vya kielektroniki. Tazama mchapishaji katika https://www.regnumbooks.net/ na wauzaji wa vitabu mtandaoni kama vile www.kobo.com na Amazon.

Timu ya uandishi ya kugundua Shahidi Asiyegawanyika,

Tinashe Mafuta, Andrea Vogt, Sally Ababa, na David Greenlee
Julai 2025.

## Kuweka uchunguzi wa Ushahidi Usiogawanyika Katika Vitendo

Tumekuwa tukizungumzia kuhusu Ushahidi Usiogawanyika, wazo la kutokutenganisha vitendo na maelezo ya injili.

Tunapoelekea mwisho wa somo letu, tafadhali anza kuzingatia maswali haya na kuandika majibu yako.

Mawazo haya ni kwa ajili ya tafakari yako mwenyewe, maamuzi, na matumizi. Majibu mazuri ni yale yanayokusaidia kutekeleza kwa vitendo yale uliyojifunza. Hata hivyo, hutahitajika kuyashiriki na wengine, lakini,

- Zangatia ni lini na jinsi gani unaweza kuyashirikisha na baadhi ya timu yako, viongozi wako, na wafanyakazi wenzako kwa wakati unaofaa.
- Pia, tutakapokutana kwa kipengele cha 11 tutakupa nafasi ya kushirikisha mawazo yako kwa wengine katika kundi.

Tafadhali majibu yako ya swali 1-4 yakusaidie kupanga mpango kazi wa utekelezaji unapojibu swali 5-6.

Tunapoendelea mbele, tafadhali kumbuka kwamba kuna watu watakuwepo kukusaidia, ikiwa ni pamoja na wawezeshaji wa kozi. Sally Ababa, kiongozi mshiriki wa huduma za kikatalisti katika eneo ana uzoefu mwingi katika maendeleo ya jamii na atafurahi kushiriki pamoja na David Greenlee ambaye alisaidia kuunda kozi hii.

1. Somo hili limeleta tofauti gani kwako?

   MAJIBU YAKO:
   ✓
   ✓
   ✓

2. Umejifunza ukweli na taarifa gani?

   MAJIBU YAKO:
   ✓
   ✓
   ✓

3. Una maswali gani ambayo hayajajibiwa?

MAJIBU YAKO:
- ✓
- ✓
- ✓

4. Je, unafikiri unapaswa kukuza ujuzi wao?

MAJIBU YAKO:
- ✓
- ✓
- ✓

5. Unafikiri Mungu anataka ufanye matumizi gani kupitia mafunzo haya? Au katika timu yako?

MAJIBU YAKO:
- ✓
- ✓
- ✓

6. Kwa namna gani utayafanyia kazi?

MAJIBU YAKO:
- ✓
- ✓
- ✓

